# Nipashe

Jumamosi Mei 20, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581316

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


UKURASA 24



## MAYELE: INAWEZEKANA KUBEBA UBINGWA CAF


SUPA JACKPOT
TZS. 1,114,965,687
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




## Samia: Tumepiga hatua uwekezaji wa nguvu kazi malengo endelevu

UKURASA 2

# Mshtuko anguko la vyombo vya habari

- **Wabunge** waitwisha 'zigo' serikali, Nape awatumia salamu ... *Uk. 2, 3, 11, 12, 13 & 14*



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha wa 2023/24, Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Mpango atoa maagizo mazito matatu benki

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji na Mwanzilishi wa Imara Tech inayojihusisha na utengenezaji wa zana za kilimo, Alfred Chengula, kabla ya kufungua semina ya wanahisa wa Benki ya CRDB jana jijini Arusha. Wengine (kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya benki hiyo, Dk. Ally Laay na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya CRDB, Tully Esther Mwambapa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wasiojulikana wateketeza kwa moto jengo la mahakama

UKURASA 3




WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI

Mpango na Bajeti ya Serikali katika Ujenzi wa Miundombinu Nchini
Kusomwa Bungeni Mei 22-23, 2023

KAA TAYARI






Rais Samia Suluhu Hassan akibonyeza kitufe kuzindua Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika kuhusu Rasilimali Watu, jijini Dar es Salaam jana. Mkutano huo, unatarajiwa kufanyika Julai 25-26 mwaka huu, jijini humo. **PICHA: IKULU**

# Samia: Tumepiga hatua uwekezaji nguvukazi SDG

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema Tanzania imepiga hatua kwenye sekta ya uwekezaji hasa katika nguvu kazi ya taifa kufikia Malengo Endelevu ya Millenia (SDG).

Kadhalika, ameiomba Benki ya Dunia (WB) kuisaidia Tanzania ili iweze kufikia malengo iliyojiwekea ifikapo mwaka 2030.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kikao cha wakuu wa nchi za Afrika, kilichokuwa na lengo la kujadili nguvu kazi. Mkutano utakaofanyika kuanzia Julai 25 hadi 26 mwaka huu.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Rais Mstaafu wa Zanzibar Dk. Ally Mohamed Shein, mawaziri, mabalozi, makatibu wakuu, wakuu wa mashirika wa kimataifa na viongozi wa ulinzi na usalama.

Pamoja na mambo mengine Rais Samia alisema baada ya Tanzania kufanikiwa kuwekeza katika nguvu kazi hivi sasa ipo tayari kuwa mwenyeji wa mkutano huo ili kushirikisha uzoefu wa namna ilivyofanikiwa.

Alisema mkutano huo ni muhimu kwa Tanzania kuzielezea nchi za Afrika umuhimu wa kuwekeza kwenye nguvu kazi kwa maendeleo endelevu.

"Tanzania imefanya vizuri katika utekelezaji wa malengo endelevu. Tunahitaji msaada kufikia safari yetu kwenye malengo ambayo tumejiwekea,"alisema Rais Samia na kuongeza:

"Uwekezaji kwenye nguvu kazi ni muhimu kuboresha maisha ya watu na kuondoa umaskini. Malengo endelevu hayawezi kutenganishwa na nguvu kazi ya taifa,".

Alisema kwa Tanzania maendeleo ya nguvu kazi imekuwa ni moja ya vipaumbele vyake katika mipango ya maendeleo.

"Hatuko katika hali mbaya kama baadhi ya ripoti zinavyojaribu kuonyesha, tumefanya kazi kubwa na tunaendelea," alisema Rais Samia.

Rais Samia alisema Umoja wa Afrika (AU) kwenye mpango wake wa agenda mwaka 2063 imeweka wazi suala la nguvu kazi kama kipaumbele chake muhimu kwa kusisitiza kuchangia huduma za elimu na afya.

Aidha, Rais Samia aliwaomba viongozi wa nchi za Afrika kuendelea kuwekeza kwenye nguvu kazi hasa vijana na kinamama.

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema mkutano huo ni jukwaa muhimu la kuwakutanisha pamoja viongozi, kujadiliana na kubadilishana uzoefu kwenye masuala yanayoleta matatizo katika uwekezaji wa nguvu kazi.

Alisema Tanzania imewekeza kwenye nguvu kazi ya taifa kwenye maeneo ya afya, elimu, maji na miubdombinu.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, alisema mkutano huo ni hatua muhimu katika kupeleka mbele ajenda ya nguvu kazi kwenye bara ya Afrika.

Alisema uamuzi wa Tanzania kuwa mwenyeji wa mkutano huo unathibitisha utayari wa nchi za Afrika na masuala ya kimataifa.

Waziri Tax alisema maendeleo ya nguvu kazi ni mafanikio kwenye uwekezaji wa ajenda ya mwaka 2063 ambayo inataka uwekezaji mkubwa na uratibu kwa nchi zote za Afrika.

Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Dk.Saada Mkuya, alisema mafanikio makubwa yamefikiwa baada ya uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye nguvu kazi ya taifa.

Mkuya alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zimeongeza bajeti zake ili kuwawezesha watu kupata huduma bora za afya, elimu na maji.

Mkurugenzi Mkazi wa WB Tanzania, Nathan Belete, alisema nchi za Afrika zinapaswa kuja na mipango na namna bora ya kuondokana na matatizo yanayoikabili nguvu kazi ya taifa.

# Mshtuko anguko vyombo vya habari

**Na Romana Mallya,** DODOMA

HUKU kukishuhudiwa anguko la vyombo vingi vya habari nchini, wabunge wameinyooshea kidole serikali, wakiitaja kuwa sehemu ya tatizo hilo.

Katika mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa mwaka 2023/24 bungeni jana, baadhi ya wabunge walisema serikali inadaiwa na vyombo vya habari karibu Sh. bilioni 30, hivyo ni sehemu ya tatizo, hivyo kusababisha vyombo vya habari kushindwa kujiendesha na wafanyakazi wanaishi kama ombaomba.

Mbunge wa Viti Maalum, Ester Bulaya, alisema kwa sasa walau wanahabari wanauona mwanga, wanapumua na wanafanya kazi kwa uhuru ambao wanauhitaji zaidi.

"Mheshimiwa Nape, unajua mimi ni mwandishi wa habari. Nimekaa chumba cha habari nilianza kama mwandishi wa habari mwanafunzi... ninajua changamoto za wenzangu.

"Asilimia 90 ya waandishi wa habari hawalipwi , hao ni kwenye sekta binafsi na wameshazoea hiyo hali na hawana mtetezi. Mheshimiwa Nape usikubali wewe kama waandishi walivyo na imani na wewe na umewapongeza kwa kazi nzuri wanayoifanya.

"Huu mhimili usionekane tu upo upo, upewe heshima yake. Waandishi wapewe hadhi yao kwa kazi kubwa wanayoifanya kuhabarisha watanzania, yaani leo mwandishi ategemee 'source' (chanzo cha habari) kumpa chochote, si kwamba anapenda," alisema.

Alisema mwandishi wa habari anatakiwa alipwe na chombo chake vizuri ili akiamua kufanya habari za uchunguzi kwa maslahi ya nchi awe na uwezo, asiwe mnyonge.

"Mheshimiwa Nape kuna vyombo vya habari miaka 10 havilipi waandishi. Kuna chombo kinadaiwa Sh. bilioni 3.5 na waandishi zaidi ya miaka 10. Kuna waandishi wengine wanadai vyombo vyao Sh. milioni 100, milioni 200, milioni 300 hawalipwi, lakini wapo huwasikii wakinung'unika. Wapo humu wanatuandika kwa kinyongo lakini hawawezi kukaa nyumbani wana familia.

"Lazima watoke wakafanye kazi labda huko wataonana na watu wenye nia njema, hii kazi si ya kujitolea ni kazi kama wakili, daktari, mwalimu wanahitaji wapate malipo yao," alisema akibainisha kuwa hata michango kwa walioajiriwa haiendi kwenye mifuko na kuhoji hatima yao baada ya kazi itakuwaje.

Pia aliongeza: "Kuna kampuni waandishi wameamua kufanya kazi tu bure hawana mikataba... mbali na magumu wanayopata hawalipwi."

Bulaya alisema leo wakichanganya vyombo vya habari vya umma na sekta binafsi serikali inadaiwa karibia Sh. bilioni 30.

"Mnapewa huduma ya matangazo hamlipi, Sahara Media anayedaiwa na watumishi wake, anasema anawadai serikali Sh bilioni sita, Daily News pekee mnadaiwa Sh. bilioni 11," alisema na kuhoji wanawezaje kufanya operesheni kutaka waandishi walipwe kama serikali hailipi matangazo.

Suala lingine alisema ni la wadau wa habari ambao wameomba kupitia mchakato wa marekebisho ya sheria ya habari kwamba usiende haraka kwenye Bunge wapate nafasi ya kutoa maoni.

Mbunge wa Jimbo la Kishapu, Boniface Butondo, alisema waandishi wa habari wengi wana shida.

"Unaweza kusema ni ombaomba japokuwa lugha ile si nzuri. Lakini tabu kubwa Mheshimiwa Nape ni mikataba kwa watumishi hawa, wengi wa waandishi wa habari hawana mikataba na wamekuwa na shida kweli.

"Maisha yao kama si sisi unapokuwa kwenye majukumu hayo ya kutuwajali na kuwapa chochote, wanaishi maisha ya tabu sana, tunaomba kwa sababu wewe ndiye baba na mlezi uwatizame na uhakikishe unawalea," alisema.

Mbunge wa Buchosa, Erick Shigongo, alisema maisha ya vyombo vya habari ni magumu.

"Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, msivipatie vyombo vya habari ruzuku , ruzuku wapeni TSN, Uhuru na wengineo. Sisi tunachokitaka na wengine huko ni vyombo vya habari vya serikali vijitoe kwenye matangazo.

"Yaani ITV wasigombanie matangazo na TBC, BBC hawachukui matangazo, Voice of America hawachukui matangazo, vyombo vya serikali visigombanie matangazo na vyombo vya binafsi," alisema.

**WIZI WA MITANDAO**

Katika mjadala huo pia, kuliibuka hoja ya utapeli mitandao ambapo Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita, aliitaka serikali iongeze nguvu suala hilo.

"Wizi wa mitandao ni janga linalowasumbua wadau wengi, tuongeze teknolojia ili wezi hawa wasiwatapeli watanzania.

Tumekuwa tukiripoti kosa kwenye kampuni za simu ambacho hatupati ni mrejesho, ni lazima kampuni za simu watuambie kama wateja kwamba 'ile simu uliyoripoti tumefanya moja, mbili, tatu' haiwezekani turipoti alafu hakuna mrejesho," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Kilimanjaro, Zuwena Bushiri alisema wezi wa 'tuma kwa namba hii jina litatoka hivi' serikali inatakiwa kuwafanyia kazi.

"Wanayofanya matapeli wanataka kuwazidi akili, msikubali wizi wa kutumia simu ukakithiri Tanzania," alisema.

**MAJIBU SERIKALI**

Akijibu hoja hizo, Waziri wa wizara hiyo, Nape Nnauye, alisema suala la maslahi ya waandishi wa habari haliwezi kutatuliwa kwa kauli za kisiasa bali kwa sheria ambayo itapelekwa bungeni ili kulinda misingi ya haki zao na kuondokana na kupewa haki kwa hisani.

Kuhusu matapeli mitandaoni, Nape alitangaza kiama chao na kuliomba Bunge liwasamehe kidogo watafumba macho kwenye mambo ya msingi kwa kuwa yanaudhi.

"Tumejipanga vizuri tutaomba ndugu zetu wa polisi ili tulifute kwenye nchi yetu," alisema.

Kuhusu serikali kudaiwa na vyombo vya Habari, alikiri ni kweli lakini kiasi kilichotajwa kinatofautiana na kwamba hesabu aliyo nayo ni Sh. bilioni 18.

Awali, Nape aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 212.457 kati ya hizo, Sh. bilioni 30.503 kwa matumizi ya kawaida na Sh. bilioni 181 miradi ya maendeleo.

HABARI KITAIFA



Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akimtunuku Shahada ya Uzamivu Dk. Wilberforce Joseph wakati wa mahafali ya 53 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, jana. Kushoto ni Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. William Anangisye. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mpango atoa maagizo matatu kwa benki

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ametoa maagizo matatu kwa benki nchini, ikiwamo kutozalisha mikopo chechefu mipya ili kuwe na uhakika zaidi na uwekezaji katika sekta hiyo.

Alitoa maagizo hayo jana alipokuwa akifungua semina maalum ya elimu ya fedha na uwekezaji kwa wanahisa wa Benki ya CRDB na umma iliyofanyika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Arusha (AICC), jijini hapa.

Dk. Mpango alizitaka benki za biashara ziendelee kuzingatia ufanisi katika utendaji, ikiwamo kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Ili kupunguza mikopo chechefu, Makamu wa Rais alisema ni muhimu menejimenti za benki zihakikishe hakuna mikopo chechefu mipya na kuzingatia ukomo wa asilimia tano uliowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

"Tatu, pamoja na kwamba maendeleo ya kidigitali yamesaidia kuwajumuisha watu wengi zaidi katika sekta ya fedha, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo hatuna budi kuzitafutia ufumbuzi.

"Kwa mfano, baadhi ya Watanzania hasa wanaoishi vijijini, hawajafikiwa au hawatumii huduma za fedha.

Ni asilimia 8.6 tu ya wananchi wanaoishi vijijini wanapata huduma za benki kwa sasa," alibainisha.

Makamu wa Rais alitaja kikwazo kilichopo ni masharti magumu na riba kubwa za mikopo. Alisema ni kikwazo kwa walio wengi kunufaika na mikopo.

"Tumeanza vizuri katika sekta ya kilimo cha mazao na kilimo biashara na sasa baadhi ya benki zinakopesha kwa riba ya asilimia tisa, ingawa ninaamini inawezekana kushuka zaidi.

Ninaziomba benki zione pia uwezekano wa kufanya hivyo kwa sekta nyingine ikiwamo wachimbaji wadogo, wafugaji wa samaki, ng'ombe, mbuzi, kuku, nyuki na wavuvi," alisema.

Katika semina hiyo iliyoambatana na maonyesho ya biashara changa za vijana, Dk. Mpango alishuhudia ubunifu wa baadhi ya vijana unaoendelezwa kupitia programu ya IMBEJU.

Alipongeza jitihada za CRDB kushirikiana na serikali kuyawezesha makundi ya kiuchumi Tanzania Bara na Zanzibar kupitia programu hiyo. Aliipongeza benki hiyo kwa mafanikio makubwa iliyoyapata katika kipindi cha miaka mitano iliyopita yaliyoshuhudia ikiendelea kutengeneza faida inayoiwezesha kutoa gawio kwa wanahisa wake.

"Nimefurahisha kusikia mwaka huu Bodi ya Wakurugenzi imekuja na pendekezo la ongezeko la asilimia 25 la gawio kwa kila hisa. Wanahisa wa Benki ya CRDB mnastahili kutembea kifua mbele kwa ongezeko hili," alipongeza na kubainisha kuwa serikali nayo itanufaika na ongezeko hilo kwa kuwa ina hisa ndani ya benki hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema dhamira ya benki hiyo ni kuifanya programu ya IMBEJU kuwa endelevu ndiyo maana wanashirikiana na wadau mbalimbali ili kuwafikia vijana na wanawake wengi zaidi.

"Tunaamini mafanikio ya programu hii yapo katika ushirikiano, ndiyo maana tangu mwanzoni tulianza kwa kushirikiana na wenzetu wa COSTECH (Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia) na ICTC (Tume ya TEHAMA) na hivi karibuni tumetia saini mkataba na Shirika la Care International," alisema Nsekela huku akiainisha kuwa mpaka sasa vijana 709 na zaidi ya wanawake 4,000 wameshanufaika na programu hiyo.

"Programu ya IMBEJU imejumuishwa katika semina ya wanahisa wa benki hiyo ili kuwaonyesha kwa vitendo mwelekeo wa mkakati mpya wa Benki ya CRDB wa miaka mitano kuanzia mwaka 2023 - 2027 ambao umejikita katika kuleta mageuzi thabiti katika biashara ya benki kupitia huduma, bidhaa na programu za ubunifu katika soko," alisema.

Mwaka huu, Benki ya CRDB imepata leseni ya kutoa huduma Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na leseni ya kampuni tanzu ya CRDB Insurance. Nsekela alisema kwa hatua hiyo, benki sasa inatoa huduma katika nchi tatu ambazoni Tanzania, DRC na Burundi ambako ilifungua tawi miaka 10 iliyopita.

# Mageuzi makubwa habari, mawasiliano

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WIZARA ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, imepanga kufanya mabadiliko na maboresho makubwa kwenye sekta ili kuendana na mageuzi kwa kuharakisha uendelezaji na usimamiaji miundombinu ya TEHAMA, Mawasiliano, Posta na habari.

Waziri wa Wizara hiyo, Nape Nnauye, aliyasema hayo jana bungeni wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24 huku ikiomba kuidhinishiwa Sh. bilioni 212.457.

Alisema baadhi ya miundombinu hiyo ni Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, anwani za makazi, mitambo ya utangazaji kwa lengo la kuchochea mfumo mpya wa uendeshaji wa uchumi wa kidijitali.

Mageuzi mengine, alisema ni kufanya mapinduzi kwenye Taasisi za Sekta; kuimarisha mashirikiano na Sekta binafsi, kuendeleza utafiti na ubunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), kuwajengea uwezo watumishi kuendana na mapinduzi hayo, kuwezesha sekta zingine kuelekea kwenye mapinduzi ya kidijitali na kuweka mazingira ya kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari.

"Wizara imekusudia kufanya mageuzi kwenye taasisi zake ili ziweze kutoa huduma zake kwa ufanisi zaidi.

Shughuli nyingine zitakazotekelezwa ili kuharakisha mapinduzi ya kidijitali na kuboresha mazingira ya wanahabari na vyombo vya habari katika maeneo mbalimbali.

"Kufanya mapitio ya Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 ili kuifanya iendane na mabadiliko katika Sekta ya Habari.

Kuendelea kutekeleza Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2017," alisema.

Pia alisema kuratibu utungaji wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) na kuanzisha redio ya Afrika itakayotangaza kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuhimiza matumizi ya Kiswahili na kujenga umoja wa Afrika.

"Ukusanya na kusambaza habari ikiwemo kuisemea Serikali kuhusu utekelezaji wa Sera, Mikakati, Programu na Miradi inazotekeleza; kuanzisha vyombo vilivyotajwa katika Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 ambavyo ni Bodi ya Ithibati ya Wanahabari, Baraza Huru la Habari na Mfuko wa Mafunzo kwa Wanahabari," alisema.

# Wasiojulikana wateketeza jengo mahakama

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MAHAKAMA ya Mwanzo Shanwe katika Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, imechomwa moto na watu wasiojulikana na kuteketeza nyaraka zote zilizokuwa ndani ya jengo hilo.

Tukio hilo linadaiwa kutokea usiku wa kuamkia juzi huku walinzi wa mahakama hiyo wakidaiwa kutokuwapo eneo lao la kazi kwa usiku huo.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Shanwe, Mustapha Kimasa, alisema jana kuwa taarifa za kuungua kwa mahakama hiyo alipewa na mtoto wake baada ya kutoka nje usiku na kuona moto unawaka, hivyo kuchukua jukumu la kutoa taarifa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Katavi, Regina Kaombwe, alisema walipokea taarifa hizo saa 6:00 usiku kutoka kwa mwenyekiti huyo na kufika eneo la tukio saa 6:27 na kukuta jengo lote limeshika moto, hivyo askari walianza mara moja kuzima moto huo.

Kaombwe alisema hadi saa 8:40 usiku, gari la zimamoto liliishiwa maji na walipiokwenda kwenye maeneo yote ya maji ya dharura hawakupata, hivyo walirudi eneo la tukio na kuomba maji kutoka kwa wananchi ambao walitoa ndoo za maji na kuendelea kuzima moto huo.

Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Jamila Yusufu, alikiri kutokea kwa moto huo na kwamba usiku huo huo, alimwagiza Katibu Tawala wa Wilaya kuwaandikia barua Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mpanda watoe maelezo ya kukosekana kwa maji ya dharura kwa maeneo yote, kitu ambacho si cha kawaida.

Gway Sumaye, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Mkoa wa Katavi, alisema mpaka sasa wamechukua hatua ikiwamo mlinzi aliekuwapo zamu siku hiyo kushikiliwa na Jeshi la Polisi kwa uchunguzi zaidi.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, alisema uchunguzi wa awali unaonyesha tukio hilo ni la kupangwa kwa kuwa jengo hilo halikuwa na umeme, hali ambayo wangehisi kuna shoti kama huduma hiyo ingalikuwapo.

Mrindoko aliahidi kuunda tume ya siku tano kuchunguza chanzo cha moto na wahusika wote na endapo watapatikana, alisema watachukuliwa hatua za kisheria.

Alisema serikali imepata hasara kubwa kutokana na kuteketea kwa jengo hilo kwa kuwa hizo ni pesa za wananchi ikiwa ni pamoja na kuungua kwa nyaraka zote na kumbukumbu zilizohifadhiwa katika mahakama hiyo.

# Jamhuri yabanwa kesi vigogo TPA

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA imeubana upande wa Jamhuri katika kesi inayomkabili aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Madeni Kipande, ikiutaka utoe taarifa kamili ya upelelezi.

Imeonya kuwa bila kufanya hivyo washtakiwa watarejeshwa polisi au Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Uamuzi huo ulitolewa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Ramadhani Rugemarila wakati kesi hiyo ilipotajwa

Wakili wa Serikali, Mossie Kaima, alidai kesi ilikuja kwa ajili ya kutajwa na kwamba jalada la kesi liko katika hatua ya mwisho ya usomwaji katika ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), Dodoma.

Kutokana na hali hiyo, Wakili Kaima aliomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa na kwamba katika tarehe hiyo atatoa taarifa ya mapitio ya faili hilo.

Wakili wa Utetezi, Karoli Fabian, akijibu maombi hayo, alidai wamechoshwa na kauli hiyo kwa kuwa si mara ya kwanza upande wa mashitaka kueleza hayo.

Baada ya kusikiliza hoja hizo Hakimu Rugemarila alisema kuwa kwa mujibu wa mwongozo wa DPP, upelelezi wa kesi hiyo ulipaswa kukamilika ndani ya siku 90.

"Shauri linakaribia kufika mwaka mmoja tangu lilipofunguliwa Juni, 2022 na hakuna ushahidi kama faili la kesi hii liko kwa DPP Dodoma linapitiwa. Mwongozo alioutoa DPP ni kwamba uchunguzi ukamilike ndani ya siku 90 kwa kesi kama hizi kubwa na zingine zisifunguliwe kama upelelezi haujakamilika.

"Kwa kuwa sina mamlaka ya kuifuta, next time kama upelelezi haujakamilika nitawarudisha washtakiwa polisi au PCCB huko mtaamua," alisema Hakimu huku akiahirisha shauri hilo hadi Juni 15, mwaka huu.

Washitakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Ununuzi, Mashaka Kisanta; aliyekuwa Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala, Peter Gawile; Mwenyekiti wa Bodi ya Ununuzi, Casmily Lujegi na Kaimu Mkurugenzi Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Kilian Chale.

Kipande na wenzake wanashtakiwa kwa uhujumu uchumi na wanakabiliwa na mashitaka matatu likiwamo la kuisababishia TPA hasara ya Dola za Marekani milioni 1.8 (sawa na Sh bilioni 4.2).

Washitakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Oktoba Mosi, 2014 na Oktoba Mosi, 2020 Dar es Salaam, walikula njama na kuisababishia TPA hasara.

Pia wanadaiwa kati ya Januari Mosi na Februari 17, 2015, wakiwa maofisa wa TPA, walitumia madaraka yao vibaya kwa kutangaza zabuni namba AE/016/2014-15/CTB/G/39 kwa nia ya kujipatia dola za Marekani 1,857,908.04 .

Wanadaiwa pia kati ya Oktoba Mosi, 2014 na Oktoba Mosi, 2020 maeneo ya TPA na maeneo mengine ya Dar es Salaam, kwa makusudi walitangaza zabuni ya Enterprises Planning Resources (ERP) bila kupata kibali cha bodi ya zabuni ya TPA, hivyo kushindwa kufuata kanuni za zabuni na hatimaye kutoa malipo ya awali ya asilimia 40 bila idhini ya bodi hiyo, hivyo kuisababishia TPA hasara ya Dola za Marekani milioni 1.8.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Kimataifa inayotoa elimu ya Uongozi, Mawasiliano, Uwekezaji na Biashara ya Toastmasters Afrika Mashariki, Emilia Siwingwa (kulia), akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa taasisi hiyo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Utafiti waonyesha ugonjwa figo tishio kiafya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, amesema utafiti umebainisha kuwa ugonjwa wa figo bado ni tishio kwa Watanzania wengi kwa kuwa inaonyesha kuwa asilimia saba ya Watanzania wanaishi na maradhi hayo.

Dk.Mollel aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Asia Halamga. Mbunge huyo, katika swali lake, alihoji hadi sasa hali ya ugonjwa wa figo ikoje nchini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanyika nchini Tanzania katika jamii, ulionyesha kuwa asilimia saba ya Watanzania wanaishi na ugonjwa wa figo ambao kwa kiasi kikubwa ulihusishwa na ugonjwa wa shinikizo la juu la damu, kisukari na maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) na UKIMWI.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri alitoa rai kwa wananchi kupima figo mara kwa mara kwa kuwa kuchelewa kutambua tatizo, madhara yake ni makubwa na gharama ya matibabu yake ni kubwa pia.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji lini hospitali za mikoa zitaanza kutoa huduma ya usafishaji figo.

"Kwa kuwa gharama za matibabu ziko juu, nini kauli ya serikali juu ya kuwasaidia wale wananchi maskini ambao hawana uwezo wa kukidhi huduma hizo za matibabu?" alihoji.

Dk. Mollel, akijibu swali hilo, alisema Sh. bilioni 270.9 ambazo zimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan, zimetumika kuleta vifaa kwa ajili ya usafishaji figo kwenye hospitali za rufani za mikoa.

"Ni kweli kuna gharama kubwa sana kwenye kutibu figo na bei yake inaweza kushuka kuanzia Sh. 150,000 hadi Sh.90,000 lakini kuna utaratibu wa msamaha kwa wanaoshindwa kulipa,"alisema.

# RC Mtaka aonya udanganyifu fidia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

Mkuu wa mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewaonya wakazi wa kijiji cha Nkomang'ombe, Ludewa mkoani hapa wanaotarajia kulipwa fidia kupisha mradi wa makaa ya mawe, kuepuka kutoa taarifa za uongo za kutolipwa baada ya kutumia fedha hovyo.

Mtaka alitoa onyo hilo juzi wakati wa kutoa elimu ya uandaaji wa ulipaji wa fidia hiyo itakayohusisha kaya 650 ambazo zinatarajia kulipwa Sh. bilioni 5.2 kupisha eneo la mradi wa makaa ya mawe.

"Unatunga uongo, mkuu wa wilaya ameshakuja mwingine huko baadaye unasema kuna watu walilipwa fidia mimi sikuwepo. Unachukua makaratasi unaweka kwenye chai ya majani makaratasi yanazeeka na ukitunga uongo wewe ni chakula cha polisi. Ukitunga uongo unaenda kuwaambia ndugu zako kasemeni baba mdogo amedanganya kalipwa yeye wewe ni chakula cha serikali," alisema.

Mtaka alisema kuna watu waliuza ardhi kwa kutegemea kwamba mradi wa makaa ya mawe hautaanza.

"Kuna watu walisema kila maneno ya hovyo. Hawakuamini kama Nkomang'ombe kuna mali lakini mvumilivu hula mbivu. Wazazi huenda hawatakula fedha hiyo lakini wako watu wanatengeneza maisha kwa sababu ya fedha hiyo. Sisi viongozi wa serikali ya mkoa tulisema tuje tuzungumze kwamba zinakuja pesa," alisema Mtaka.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Njombe, Deo Sanga, alisema uwekezaji huo ni dhamira ya serikali katika kuinua uchumi wa taifa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe, Judica Omari, alisema wananchi 650 wanaufaika na kulipwa fidia na kuwataka wanawake kuhakikisha fedha zikipatikana wanasimamia uwekezaji.

Meneja wa CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Jenifer Tondi, alisema benki hiyo ina wajibu wa kutoa elimu ya fedha bure ili kuleta tija kwa wateja.

# Waonywa kukwamisha maboresho afya

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema haitawafumbia macho watendaji wa afya wanaokwamisha jitihada za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha sekta ya afya.

Akizungumza jana katika kikao kazi cha watendaji wa Kanda ya Ziwa kwa mikoa ya Mwanza, Simiyu, Mara Geita na Shinyanga na Bohari ya Dawa (MSD), Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Msalika Makungu, alisema lengo la Rais kufanya maboresho ya sekta hiyo ni kumpatia huduma bora mwananchi.

Kwa mantiki hiyo, alisema watendaji wanapaswa kutambua wajibu walio nao katika kufanya kazi kwa weledi na kumsaidia kufikia lengo lililowekwa.

Alisema viongozi wa mikoa katika kanda hiyo, hatawafumbia macho watendaji wanaokwamisha jitihada hizo kwa makusudi.

Makungu alisema kikao kazi hicho ni muhimu kwa watendaji ili kuwakumbusha wajibu wao katika kufanya kazi kwa weledi na kuwa sehemu ya mabadiliko kwa kutoa huduma nzuri kuanzia katika mapokezi ya wagonjwa, lugha na kuwa na matumizi sahihi ya dawa na vifaa tiba.

"Ni muhimu wataalamu watimize majukumu yao kwa weledi na huduma ziwafikie wananchi kwa kuwa sekta ya afya ni mtambuka yenye tija katika utekelezaji wa malengo ya mpango wa serikali kijamii na kiuchumi,"alisema.

Meneja wa MSD Kanda ya Ziwa, Egidius Rwezaura, alisema hivi karibuni wanatarajia kupokea vifaa vya afya zikiwamo dawa na vifaa tiba aina 100, vitanda na mshine za maabara ambavyo vitamaliza changamoto ya mahitaji yaliyopo.

Pia alisema mkakati ni kuwapo vifaa vingine vingi vya akiba katika bohari, kufikia lengo la Rais Dk. Samia katika maboresho ya huduma katika sekta ya afya.

Mfamasia Mratibu Kiongozi wa Huduma za Bidhaa za Afya kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mathew Mganga, alisema watendaji hao watambue kuwa Rais ametoa fedha nyingi kwa ajili ya dawa na vifaa, hivyo ni vyema zitumike katika ununuzi wa bidhaa hizo na si matumizii mengine.

Alisema lengo la maboresho sekta hiyo ni kufanikisha huduma bora kwa wananchi na kwamba bado fedha zinazomiminika na hatua zilizochukuliwa na serikali ya Rais Dk.Samia haiendani na huduma bora wanazopatiwa wananchi hivyo ni lazima kuchukua hatua.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara, Dk. Zabron Masatu, alisema wamepokea maelekezo hayo wataenda kubanana ndani katika utendaji kuweza kufikia lengo la Rais katika maboresho ya huduma bora za afya kwa wananchi.



Mmoja wa wakulima wa kijiji cha Kipara Mnero, wilayani Nachingwea, mkoani Lindi, akimwonyesha Mkuu wa wilaya hiyo, Mohamed Moyo (kushoto), aina ya mizizi wanayotumia kama vyakula baada ya tembo kuharibu mazao yao, wakati wa mkutano wa hadhara kijijini hapo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM.**

# Wenye ulemavu 360 Dar, Singida wanufaika na uwezeshaji kiuchumi

**Na Beatrice Philemon**

WATU 360 wenye ulemavu kutoka Dar es Salaam na Singida, wanatarajia kunufaika na mradi wa Uwezeshaji Kiuchumi Kwa Watu wenye Ulemavu wenye thamani ya Sh. bilioni moja.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira Na Watu Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi, alisema hayo wakati akizindua mradi huo jijini Dar es Salaam juzi.

Mradi huu umeanzishwa na Shirika la Sightsavers, Shirika la Kimataifa lenye makao makuu Uingereza, lililojikita kwenye sekta za afya kwa maana ya afya ya macho na magonjwa yasiyopewa kipaumbele.

Alisema lengo la mradi ni kuhakikisha soko la ajira linakuwa jumuishi kwa watu wenye ulemavu, kuleta matumaini kwa watu hawa na pia kuongeza ujumuishi kwenye mnyororo wa thamani kwenye sekta ya kilimo.

Ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wananufaika na soko la ajira, aliomba waajiri kutoka serikalini na sekta binafsi kuhakikisha kila asilimia 20 ya walioajiliwa, asilimia tatu iwe watu wenye ulemavu.

"Kama serikali tunaomba muwe watu wa mfano, nendeni mkatende kazi kwa kugusa maisha ya walengwa ili tuweze kushawishi wadau wengine waje kusaidia watu wenye ulemavu kwa sababu serikali haiwezi kufanya kazi pekee. "Hadi sasa kuna idadi kubwa ya watu wenye ulemavu wanaohitaji msaada kwa hiyo mkiweza kufanya mradi vizuri mtavutia wadau wengi kuwekeza katika eneo hili," alisema. Kwa mujibu wa Katambi, ili kusaidia watu wenye ulemavu kupata huduma stahiki, hivi sasa ofisi ya Waziri Mkuu imefanya utambuzi wa watu wenye ulemavu na kuanzisha Mfuko wa Watu wenye Ulemavu ili waweze kupata stahiki zao na hadi sasa wamefanikiwa kufungua akaunti Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Naibu Waziri huyo alisema serikali imefanya mpango mkakati wa kufungua na kujenga vyuo vya watu wenye ulemavu, ili kusaidia watu hawa kupata elimu bora ambayo itawasaidia kuingia kwenye soko la ajira au kujiajiri.

Mkurugenzi wa Sightsavers, Godwin Kabalika, alisema mradi huo ni wa miaka miwili (2022-2025) ambao utatekelezwa na Sightsavers kwa kushirikiana na serikali, Shirika la Watu wenye Ulemavu linaloshughulika na masuala ya kisheria, maendeleo ya jamii na kiuchumi (DOLASED), Sauti ya Wanawake wenye Ulemavu Tanzania (VODIWATA), Chama cha Watu Wenye Ualbino (TAS) na Taasisi ya Vijana Wenye Ulemavu (YOWDO).

Alisema lengo la mradi ni kijifunza namna sahihi na kuboresha kwa pamoja mazingira rafiki ya ajira kwa watu wenye ulemavu katika sekta za kilimo biashara na ajira za ofisini.

Kabla ya kuanzisha mradi huo, alisema walifanya utafiti uliowashirikisha wadau kwa lengo la kuangalia soko la ajira nchini kwa watu wenye ulemavu, na kwamba walitumia matokeo kutengeneza mradi huo.

"Tathimini ilionyesha kuwa soko la ajira kwa watu wenye ulemavu hawashirikishwi ... kupitia mradi huu tutawajengea uwezo waajiri, ili kusaidia watu wenye ulemavu kushiriki kwenye soko la ajira na pia kwenye mnyororo wa thamani katika sekta ya kilimo, kuunganisha wanufaika na wadau mbalimbali, ili kupata soko ya bidhaa za vitu watakavyokuwa wanazalisha,"alisema.

"Ili mradi ufanikiwe, tunahitaji ushirikiano kutoka kwa watu waliopo kwenye mradi, mradi ukiwa mzuri tuwataweza kuwa na miradi mikubwa na pia itafungua miradi mingine mikubwa ya uwezeshaji uchumi kwa watu wenye ulemavu," alisema.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi kutoka Taasisi ya Vijana Wenye Ulemavu (YOWDO, Rajab Mpilipili, alisema mradi umekuja kwa muda mwafaka kwa vijana wenye ulemavu.

"Sisi vijana tutahakikisha mradi huu unaleta matokeo mazuri kwa walengwa. Mradi utawajengea uwezo waajili kujua namna gani ya kuajili au kufanya kazi na watu wenye ulemavu na pia watu wenye ulemavu watapewa soft skills namna ya kuzitafuta ajira na namna ya kujiajiri au kuzitafuta ajira," alisema.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Yanga kutinga fainali michuano ya CAF

**HONGERA** sana Yanga kwa kufanikiwa kutinga hatua ya fainali ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu.

Mashindano hayo ni ya pili kwa ukubwa katika ngazi ya klabu baada ya Ligi ya Mabingwa Afrika, yanaandaliwa kila mwaka na Shirikisho la Soka Afrika (CAF). Yanga sasa itakutana na USM Alger, mechi ya kwanza ikichezwa Mei 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na marudiano yakitarajiwa kufanyika Juni 3, mwaka huu nchini Algeria.

Yanga ambao walikuwa ni wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye michuano hiyo ya kimataifa, waliendа kukamilisha ndoto zao za kucheza fainali baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 nyumbani walipowakaribisha Marumo Gallants FC ya Afrika Kusini, lakini ikaendeleza ubabe kwa kupata ushindi kwenye mchezo wa mkondo wa pili, ilishinda magoli 2-1. Hata hivyo safari ya Yanga katika michuano hiyo ya CAF msimu huu ilianzia katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini ilitolewa mapema na kuhamia kwenye michuano hii.

Wawakilishi hao pekee waliokuwa wamebakia katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, walienda Afrika Kusini wakiwa hawana presha ya kutetea taji la Ligi Kuu ya Tanzania Bara, kwa sababu walifunga hesabu zao pale walipowachapa Dodoma Jiji FC mabao 4-2 na kufikisha pointi 73, ambazo hazifikiwi na timu nyingine yoyote kwenye ligi hiyo.

Imeipita miaka 30 kwa timu kutoka Tanzania ambayo sasa inaongozwa na Rais. Dk. Samia Suluhu Hassan, kutinga hatua hiyo ya fainali, mara ya kwanza kwa taifa kutoa timu katika hatua hiyo ilikuwa ni mwaka 1993, ambapo Simba ya Dar es Salaam ilicheza dhidi ya Stella Abidjan kutoka Ivory Coast. Kufika fainali ni hatua kubwa kwa timu husika pamoja na nchi. Kwa sababu kila timu inaposhiriki mashindano hutamani kuona inachukua kikombe cha michuano husika au basi inacheza fainali, hatua ambayo msimu huu imefikiwa na Yanga kutoka Afrika Mashariki.

Nipashe inarudia tena kuipa Yanga hongera kwa hatua ambayo imefika. Inafahamika wazi wawakilishi hao hawajafika hapo kwa miujiza, ni maandalizi mazuri yaliyofanywa na viongozi wa klabu hiyo kuanzia kwenye mchakato wa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu, kujituma kwa nyota wenyewe, ushirikiano wa benchi la ufundi na sapoti kutoka kwa wanachama wote. Umoja na ushirikiano huu, umesaidia kufika hatua hii, lakini tutakuwa hatuna fadhila kama tutaacha kumpa pongezi za dhati, Rais Samia kwa hamasa aliyokuwa anaitoa kwa timu (Simba na Yanga), kwa kununua kila bao, alifanya hivyo kwa kutaka kuona wachezaji wanafunga mabao mengi ambayo si yatawapa fedha, lakini yatawaisia kuwafanya wasonge mbele na hatimaye kuchukua ubingwa.

Na katika kuonyesha hajawaacha njiani, Rais Samia ameahidi ametoa ahadi ya kuwapa ndege ya serikali kuelekea Algeria katika mechi ya marudiano, kwa maana wawakilishi hao wa nchi wasipate tabu na mahangaiko ya kuunganisha ndege kufika katika kituo cha mechi, kama ambavyo hufaamika ili kufika kwa waarabu hao.

Pia Rais Samia amesema atatoa Sh. milioni 20 endapo watapata ushindi, huo ni mwendelezo wa kutaka kuona Tanzania inamaliza historia ya kuwa wasindikizaji katika mashindano hayo na msimu huu kubeba ubingwa.


Yanga huu ni wakati wenu wa kuthibitisha mmefika fainali kwa uwezo wenu, hivyo mnatakiwa kupambana na kuhakikisha mnamaliza kazi mliyoianza, inawezekana na kwa kutwaa ubingwa wa Afrika, tayari mtajiwekea rekodi ya kuwa klabu ya kwanza ya Tanzania kushinda ubingwa wa Afrika, inawezekana, hakikisheni mnapata matokeo mazuri hapa nyumbani na kwenda Algeria kukamilisha kibarua.

Pia tunapenda kuchukua nafasi hii kuwakumbusha mashabiki wa soka kuacha tofauti zao na kujitokeza kwa wingi kuishangilia Yanga lakini pia kuiombea dua ya kushinda kombe hilo tena ikiwa kwenye ardhi ya ugenini kama walivyofanya Stella Abdijan kukabidhiwa kikombe na Rais Mstaafu, Ali Hassan Mwinyi baada ya kuifunga Simba.

Kila la heri Yanga katika kupeperusha vyema bendera ya Tanzania kwenye michuano ya CAF msimu huu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Muungwana Lazima Nilonge

# Kanuni za 'Play Off' nchini zahitaji maboresho kidogo

Na Adam Fungamwango

**NIMEONA** msimu huu mechi za mchujo 'Play Off' zipo tofauti na za misimu iliyopita na hii ni baada ya wadau kushauri sana kiasi cha kufanyiwa marekebisho.

Miaka kadhaa iliyopita tangu kuanza kucheza kwa mechi za mchujo, tulikuwa tukishuhudia timu za Ligi Kuu zikicheza moja kwa moja na zile zilizoshiriki Ligi ya Championship.

Mfano, baada ya kumalizika kwa msimu wa 2019/20 zilichezwa mechi za mchujo kati ya timu za Ligi Kuu na Championship.

Geita Gold ambayo ilikuwa Championship ilicheza dhidi ya Mbeya City ya Ligi Kuu, na Ihefu iliyokuwa Championship ilipangwa na Mbao FC iliyokuwa Ligi Kuu.

Na ndivyo ilivyokuwa mpaka pale wadau walipotoa maoni ya kutoridhishwa na hilo, kwani mara nyingi timu za Championship zilikuwa zikiangukia pua.

Wadau wa michezo wakaonekana kuzionea huruma zaidi timu ambazo zimepambana sana katika ligi ngumu ya Championship na kushika nafasi ya tatu au ya nne, lakini zinashindwa kupanda Ligi Kuu kwa sababu zinakutana na timu ambazo japo hazijafanya vyema, lakini zina uzoefu.

Msimu huu hali si hivyo. Bodi ya Ligi imeamua kusikiliza vilio ya wadau wa soka, na sasa timu za Championship zitapambana zenyewe na zile za Ligi Kuu nazo zitacheza zenyewe na washindi wa hapo ndiyo watapambana kusaka timu itakayocheza Ligi Kuu, iwe imepanda au imebaki.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Pamba FC ambayo ilishika nafasi ya tatu kwenye ligi ya Championship Jumapili ijayo itakuwa ugenini Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma kucheza dhidi ya wenyeji Mashujaa FC, timu ambayo ilimaliza ligi hiyo ikiwa katika nafasi ya nne.

Halafu timu zitakazomaliza nafasi ya 13 na 14 kwenye Ligi Kuu nazo zinatarajia kucheza 'play off' yao Mei 31, na marudiano yatakuwa ni Juni 3, mwaka huu.

Hapa ina maana timu moja ya Championship itacheza na timu moja ya Ligi Kuu, tofauti na zamani ambapo zingeweza kukutana timu zote za Ligi Kuu kitu ambacho wadau wengi walikuwa hawakipendi.

Tuwapongeze Bodi ya Ligi ya TFF kwa kuwa wasikivu kwa wadau na mara kwa mara wamekuwa wakisikiza mashabiki wa soka wanataka nini kwa ajili ya manufaa ya timu.

Hata hivyo mimi nadhani mechi nyingi za mchujo ni kuongeza gharama kwa bodi yenyewe pamoja na klabu ambazo zimekuwa zikiingia gharama za kusafiri mwezi mzima.

Mfano Pamba italazimika kwenda Kigoma kucheza na Mashujaa, hivyo hivyo wapinzani wao, halafu baada ya hapo wana kibarua tena cha gharama ya kusafiri kucheza mechi na timu inayotoka Ligi Kuu.

Nia ni nzuri, lakini nadhani kuna vitu vingine vinaonekana havina umuhimu sana. Katika kuboresha kanuni msimu ujao ikipendeza ni mshindi wa tatu wa Championship, moja kwa moja acheze mechi ya mchujo na atakayeshika nafasi ya 14 kwenye Ligi Kuu.

Ukiangalia mlolongo wa mechi zote hizi ni nafasi inayohitajika ni moja tu. Zinaposhuka timu mbili kwenye Ligi Kuu, inayobakia ni nafasi moja inayoshika nafasi ya 14 inaweza ikabaki au ikashuka daraja.

Katika Ligi cha Championship baada ya kupanda daraja timu mbili moja kwa moja, inayohitajika hapo ni nafasi moja tu ya kupanda au kubaki hapo hapo.

Kwa maana hiyo wala sioni haja ya kuwa na lundo la mechi. Badala yake timu ya tatu upande huu na ile ya nafasi ya 14 upande mwingine zipige mechi mbili za 'play off' kugombania nafasi moja iliyobaki, basi.

Nadhani hii itapunguza hata muda kwa sababu baada ya ligi kumalizika, wachezaji wanahitaji mapumziko, na hata wao wenyewe wanakuwa na dili za kuhama au kuhamia klabu nyingine. Wakati mwingine tuwahurumie wachezaji wetu kwa sababu wanacheza mechi zinazokaribiana na muda mrefu pamoja na gharama kwa klabu ambazo nyingi ziko hoi.

MAKALA MAALUM

# Historia mpya uzinduzi Ikulu Chamwino

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kuzindua Ikulu ya Chamwino ikiwa ni miaka kadhaa tangu Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, alipotangaza rasmi kutekeleza uamuzi wa serikali kuhamia Dodoma. Hatua hiyo ni kukamilika kwa safari iliyochukua zaidi ya miaka 40 ya serikali kuhamishia makao makuu ya nchi mkoani Dodoma.

Katika kila awamu tangu ile ya kwanza chini ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere hadi awamu ya nne chini ya Rais (mstaafu) Dk. Jakaya Kikwete, serikali ilijitahidi kuhamishia baadhi ya wizara na taasisi za kisekta Dodoma.

Mfano, katika awamu ya kwanza, baadhi ya vikao vya Bunge, isipokuwa Bunge la Bajeti vilikuwa vikifanyikia Dodoma kabla ya miaka kadhaa baadaye mhimili huo kuhamia moja kwa moja mkoani hapa. Baadaye ikatangazwa Ofisi ya Waziri Mkuu kuhamia Dodoma licha ya kwamba ofisi ya Magogoni ilikuwa bado inafanya kazi.

### TULIKOANZIA

Mwaka 1973, serikali iliazimia kuhamishia makao makuu ya nchi kuwa Dodoma kutoka Dar es Salaam na utekelezaji wake ungefanyika ndani ya kipindi cha miaka 10 (hadi mwaka 1983) lengo likiwa kurahisisha utoaji wa huduma kwa jamii.

Oktoba 10, 1973 Mwalimu Nyerere alitangaza uamuzi wake wa kuhamishia Ikulu Chamwino, Dodoma na kujenga makazi yake na wizara kadhaa ikiwamo Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Katika uamuzi huo, Nyerere alianzisha Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu (CDA) ili kufikia azma hiyo.

Aidha, serikali ya awamu ya tatu chini ya Rais Hayati Benjamin Mkapa ilitangaza kuhamishia Wizara ya Ushirika na Masoko chini ya aliyekuwa Waziri, Sir George Kahama, na ile ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Mitaa). Chini ya Hayati Kingunge Ngombale Mwiru kuhamia Dodoma, ikiwa ni utekelezaji wa azma ya serikali kuhamia rasmi Dodoma.

### UAMUZI KAMILI

Baada ya kuingia madarakani, Julai 2016, wakati wa Siku ya Mashujaa iliyofanyika kwa mara ya kwanza Dodoma, Dk. Magufuli alitangaza kwamba serikali yake inahamia rasmi Dodoma. Miezi miwili baadaye, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alihamia rasmi.

Ni uamuzi ambao umezaa matunda ya uwekezaji mkubwa wa miundombinu uliofanyika na unaoendelea kwa sasa ikiwamo ujenzi wa awamu ya pili ya majengo ya ghorofa kwenye Mji wa Serikali, Mtumba, na kukamilika kwa ofisi muhimu ya Rais, Ikulu ya Chamwino.



Rais Samia Suluhu Hassan

Kamanda wa Operesheni ya Ujenzi huo kutoka Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Samwel Jambo, anasema kazi ya ujenzi ilikabidhiwa rasmi kwao Januari, 2020 na ilizinduliwa Mei 2020 na Rais Magufuli.

"Hadi sasa ujenzi huu umekamilika kwa asilimia 100 na uko tayari kukabidhiwa kwa Rais Mei 20, 2023. Ujenzi huu umetekelezwa na maofisa na askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) pamoja na vijana wa JKT wakiwamo watumishi wa umma. Tumeshiriki kwa pamoja kutekeleza mradi huu," anasema.

Anasema ujenzi huo umefanywa na vijana wazawa ambao umri wao hauzidi miaka 40 na usanifu umefanywa na vijana kutoka Wakala wa Majengo Tanzania (TBA).

"Tunamshukuru Rais na serikali kwa kutuamini kutekeleza mradi huu ambao umejengwa kwa viwango vinavyotakiwa. Majengo yaliyojengwa ni kama yale ya Dar es Salaam, yamehamishwa kama yalivyo," anasema.

### HISTORIA ZA IKULU

Ikulu ya Dar es Salaam ilijengwa kabla ya vita vya kwanza vya dunia ikiwa chini ya msanifu John Sinclair. Ikulu hiyo ilijengwa chini ya utawala wa Wajerumani, hata hivyo wakati Waingereza wakimtoa Mjerumani, baadhi ya majengo yalipigwa bomu.

Mwaka 1920, Waingereza wakiwa wanaitawala Tanganyika wakati huo, walianza kujenga makazi ya gavana katika majengo hayo. Pia waliongeza majengo mengine ya utawala.

Hata hivyo, kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi, Ikulu ya Dodoma inajengwa na vijana wazawa kutoka Jeshi la kujenga taifa (JKT). Eneo la Ikulu hiyo lina ukubwa wa ekari 8,473 ikiwa imezungukwa na ukuta mrefu wa kilometa 27, hivyo kuwa ukuta mrefu zaidi ya uliojengwa katika eneo la madini la Mererani.


Muundo wa majengo yatakayojengwa yatafanana kama yalivyo majengo ya Ikulu ya Dar es Salaam, kwa kutumia teknolojia ya Mjerumani, Mwingereza na mu- Asia.

Kama ilivyokuwa ada, katika Ikulu hiyo ya Chamwino kuna wanyamapori mbalimbali wakiwamo pundamilia, swala, sungura, digidigi, twiga na tausi 544.

### HISTORIA IKULU CHAMWINO

Aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa kijiji cha Chamwino Ikulu, ambaye kwa sasa ni Diwani wa eneo hilo, Joseph Seganje, anasema ni miongoni mwa vijiji hapa nchini vilivyoasisiwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Nyerere.

Kijiji hicho kilianza kutokana na kambi ya vijana kilichokuwa chama tawala cha Tanganyika na baadaye Tanzania, Tanganyika African National Union (TANU), yaani TANU Youth League (TYL) lililokuwa kitongoji cha Ipala Lyanhembo (Fuvu la Tembo) na kambi hiyo iliongozwa na mwenyekiti wake, Mzee Robina Ligoha.



Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

Hayati Mwalimu Nyerere alitembelea kambi hiyo Mei 5, 1969 kuona shughuli za uzalishaji wa zabibu, ukakamavu na utamaduni. Katika hotuba yake kambini hapo, alitoa agizo kwamba Watanzania wasiishi kama panzi, bali waishi kama nzige.

Seganje anasema tarehe hiyo hiyo yaani Mei 5,1969 hayati Mwalimu Nyerere alipanda mlima wa Matingha ambao siku hizi unajulikana kwa jina la Mwongozo palipojengwa Ikulu ya sasa ya Chamwino pia kuna nyumba ndogo mlimani ilijengwa kwa kumbukumbu yake kwa kupanda mlima huo.

"Alipopanda mlima huo alipendezwa na mandhari aliyoiona ilivyomvutia, aliangalia mteremko wa mlima pande zote, alishauri kambi ya vijana wa Tanu Youth League kuhama kutoka kitongoji cha Ipala Lya Nhembo kuja kitongoji cha Makungulu Chamwino ambapo kwa sasa ni kijiji cha Chamwino Ikulu," anasema Seganje.

Vijana wa kambi hiyo waliitikia wito, hivyo mwaka 1970 kambi hiyo ilihamia mahali alipoainisha Baba wa Taifa na kusema hapo panafaa. Pia nyumba zisizopungua 10 nazo zilikuwa mstari wa mbele kuhamia mara baada ya agizo hilo.

Aidha, Julai 10, 1971 Baba wa Taifa alifika rasmi kuzindua kijiji hicho na alikaa kwa muda wa miezi mitatu hadi Oktoba 30, 1971 akiishi kwenye hema na kuhakikisha wananchi wanaanza kuhamia.

Pia Julai 11, 1971 alianza shughuli za kufyatua matofali ya nyumba za wazee na wasiojiweza kwa balozi wa kwanza, Leng'aisi Mayai.

Mzunguko wa shughuli alizofanya baba wa Taifa kupangiwa mabalozi mbalimbali katika kijiji kwa kufyatua matofali na kujenga nyumba pia.

Baba wa taifa pia alishiriki kuchimba mitaro kwa ajili ya usambazaji wa maji kijijini.

Shughuli zingine zilizofanyika ni kusimamia makatapila kufyeka miti maeneo ya mashamba, mbuga ya Madyma ambapo waligawiwa wananchi kulima eneo hilo na pia kuna mbuyu uitwao Mwalimu J.K Nyerere kwa kumbukumbu yake, sehemu aliyofanyia mkutano na wanakijiji.

Nyerere pia alishiriki kufyatua matofali yaliyotumika kwa ujenzi wa Ikulu ndogo iliyojengwa mwaka 1971. Hivi sasa nyumba hiyo inatumika kama nyumba ya wasaidizi wa Rais na huduma mbalimbali za kijamii kwa kutumia mashine iliyotoa matofali 12 kwa wakati mmoja.

Huduma nyingine za kijamii zilizofaidika na matofali hayo ni kama kujengea ukumbi wa kijiji, wenye ofisi za watendai wa kijiji, zahanati, shamba la mifugo ya ng'ombe wa kisasa wa maziwa, ufugaji wa mbuzi wa kisasa, kuku wa kisasa, nguruwe, josho la mifugo, nyumba za watumishi wa serikali ya kijiji.

Aidha, Nyerere alishiriki kujenga nyumba za matofali ya kuchoma kwa wanakijiji.Pia alishiriki kucheza bao na wazee kwenye mti wa Mnyinga uliopo kitongoji cha Kambarage baada ya saa za kazi mti huo upo hata sasa.

Kijiji hicho kilianza na vitongoji sita vya Kambarage, Mwongozo, Umoja, Maendeleo, Azimio na Ukombozi.

Majina hayo yote hayati baba wa taifa aliyabuni na kuvipatia majina hayo.



Ikulu ya Chamwino




Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) Taaluma, Dk. Nasib Rajabu (kushoto), Kaimu Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Profesa Tandi Lwoga (wa pili kushoto) na Makamu Mkuu wa chuo hicho, Utawala na Fedha, Prof. Emmanuel Munishi wakimsikiliza Mhadhiri wa Idara ya Vipimo na Viwango, Faraja Edward (kulia) wakati akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu Siku ya Vipimo Duniani inayoadhimishwa leo. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# CBE yahamasisha vijana elimu ya viwango

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimewataka wazazi nchini kuwahamasisha watoto wao kuchangamkia mafunzo ya sayansi ya vipimo na viwango kwa kuwa soko la ajira liko wazi kwa nchi za Afrika Mashariki.

Hayo yalisemwa jana chuoni hapo na Kaimu Mkuu wa Chuo, Prof. Tandi Lwoga, wakati akizungumzia Siku ya Vipimo Duniani ambayo huadhimishwa kila Mei 20 ya kila mwaka.

Kaulimbiu ya maadhimisho hayo kwa mwaka huu ni "Vipimo Vinavyosaidia Mfumo wa Chakula Duniani" na inasisitiza jukumu muhimu ambalo vipimo vinafanya katika kuhakikisha ubora na usalama wa chakula.

Alisema kozi hiyo inatolewa na chuo hicho pekee kwa nchi za Afrika Mashariki, hivyo kuwa rahisi kwa wanafunzi wanaohitimu kupata ajira kwenye nchi zinazoizunguka Tanzania na duniani kwa ujumla.

Prof. Lwoga alisema chuo hicho kimekuwa kikitoa mafunzo hayo kuanzia ngazi ya cheti, stashahada na shahada ya sayansi ya vipimo na kwamba kwa sasa kuna wanafunzi 761 wanaosomea kozi hiyo. Alisema wamekuwa wakifanya utafiti kuhusu ubora wa miundombinu pamoja na kutambua maeneo ya kukuza teknolojia na njia mpya ya za upimaji wa bidhaa mbalimbali.

"Pia tumekuwa tukiboresha mitaala na mwaka jana. Tuliboresha mitaala ili iendane na sayansi na teknolojia ya vipimo na viwango duniani kwa hiyo tunakaribisha mlete vijana wenu waje kusoma haya mafunzo ambayo tumeyaboresha zaidi," alisema.

Pia alisema wamekuwa wakitoa mafunzo hayo kwa vitendo na kwamba wameanzisha mradi wa ujenzi wa ghorofa 10 ambalo litaitwa 'Metrology Complex' na kutakuwa na maabara ya kisasa ambayo itathibitishwa kimataifa ili kutoa mafunzo.

Alisema watakuwa pia kutakuwa na karakana ambapo wanafunzi wa sayansi ya vipimo watakuwa wakisoma kwa vitendo ambapo pia kutakuwa na kumbi za mihadhara na kwamba jingo hilo litakauwa na uwezo wa kuchukua zaidi ya wanafunzi 4,460.

Alisema lengo ka kusherehekea Siku ya Vipimo Duniani ni kunatambua umuhimu wa vipimo sahihi kwenye biashara duniani.

Wakati idadi ya watu duniani inafikia bilioni nane, alisema ni muhimu zaidi kuliko wakati wowote kuhakikisha kuwa usambazaji wa chakula na bidhaa mbalimbali ni salama.

"Tunakabiliwa na changamoto zinazozidi kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na sababu nyingine za mazingira, ni muhimu zaidi kuliko wakati wowote kuwa na vipimo sahihi na vya kuaminika," alisema.

Alisema CBE itaadhimisha Siku ya Vipimo Duniani kama nchi zingine na kwamba watakuwa na matukio na shughuli mbalimbali zinazoonyesha umuhimu wa vipimo sahihi.

Mkuu huyo alitaja shughuli hizo kuwa ni pamoja na semina, warsha, maonyesho, na mihadhara ya umma kwa kwa kushirikiana na wanasayansi, wataalamu wa vipimo na viwango kote

# Machinga kutambuliwa wafanyabiashara rasmi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inaandaa utaratibu wa kuwatambua wamachinga waliofuzu kuwa wafanyabiashara baada ya kurasimisha biashara zao.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji wamachinga wangapi wamefuzu kuwa Wafanyabiashara rasmi kwa kipindi cha mwaka 2016 hadi 2021.

Akijibu swali hilo, Kigahe alisema hadi Machi, mwaka huu, kuna wamachinga 1, 987,361 nchini.

Naibu Waziri alisema serikali inaendelea kuhamasisha urasimishaji wa biashara nchini kupitia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya faida za urasimishaji biashara kupitia mafunzo mbalimbali ya biashara na ujasiriamali.

"Mikakati iliyopo kwa sasa ni uanzishaji wa vituo jumuishi vya urasimishaji wa biashara na uandaaji wa mwongozo wa taratibu za kurasimisha biashara nchini,"alisema.

# Watumishi 2,000 umma washtakiwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2020 watumishi wa umma 2,060 walifikishwa mahakamani na kushtakiwa kwa makosa mbalimbali ya rushwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329.

Kati ya watumishi hao, 863 walishinda kesi na kuachiwa huru na waendelee na kazi.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mikumi (CCM), Dennis Londo.

Mbunge huyo alihoji watumishi wangapi wa umma wamefikishwa mahakamani kwa rushwa, wangapi wameshinda kesi na kurejeshwa kazini kwa kipindi cha 2010 hadi 2020.

Kikwete alisema kati ya watumishi hao 2060 walioshtakiwa, watumishi 1,157 walitiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu mbalimbali kwa mujibu wa sheria.

# DED apewa wiki tatu utwaaji ardhi Kilosa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, Wilfred Sumari, ametoa wiki tatu kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, kuhakikisha mchakato wa makabidhiano na uchukuaji wa ekari 2,500 katika shamba la mwekezaji aliyekuwa Mbunge wa Bukoba Vijijini, Nazir Karamagi, unakamilika ili kupisha maendeleo.

Sumari alitoa agizo hilo kwenye kikao cha kawaida cha baraza la madiwani cha robo ya tatu ya mwaka baada ya madiwani wa halmashauri hiyo kuridhia kuchukua ekari 2,500 badala ya 3,000 walizotaka kuchukua awali kutoka kwenye shamba la mwekezaji huyo na wenzake ili kutoa nafasi kwa mwekezaji kubaki na hekari 10,000.

Mwenyekiti huyo alisema halmashauri ina mpango wa kuongeza vyanzo vya mapato baada ya serikali kuhamisha mapato ya nyumba za kulala wageni na kuyaingiza kwenye hoteli za kitalii.

Alisema jambo hilo lilisababisha kushuka kwa ukusanyaji mapato mwaka huu kwa asilimia 76 baada ya kukosa zaidi ya Sh. milioni 101.

Alisema tayari wameshaanza kuona namna ya kujipanga kuongeza vyanzo vya mapato wakianzia na kujenga stendi ya mabasi na maegesho ya malori Dumila.

Sumari alisema wameshaandika barua kuomba kurudishiwa baadhi ya nyumba za kulala wageni kwa sababu hazina hadhi ya kuwa hoteli za kitalii licha ya kuingizwa katika mfumo huo na kusababisha kukosa mapato waliyopata awali kwa ajili ya maendeleo ya wilaya.

Mmoja wa madiwani walioridhia marekebisho hayo, Amani Sewando, alisema hawaoni sababu ya kuendelea kubaki na msimamo wao bali wanamwachia mwekezaji abaki na ekari anazotaka, zitakazomfanya kuendeleza kilimo, kujenga kiwanda na kuwa nguzo ya kuongeza mapato na kukuza uchumi wa wilaya.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Kisena Mabuba, alisema eneo kamili lililoko katika kata ya Magomeni ni ekari 13,000 lakini ekari 500 zilichukuliwa na wananchi na kujengwa miundombinu isiyohamishika, hivyo serikali kusema pasiguswe na mwekezaji kubaki na hekari 12,500 wakati wakataka ekari 3,000 na mwekezaji kutaka ekari 10,000 ndipo kulipozuka maswali.

Alisema ujenzi wa kiwanda cha korosho na kuanzisha mashamba vitasaidia kutoa ajira kwa wananchi, kuhamasisha ulimaji wa korosho kama zao jipya ndani ya wilaya na kuongeza mapato sababu mwaka huu pekee katika ekari chache zilizolimwa na mwekezaji, halmashauri imepata zaidi ya Sh. milioni 14.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Shaka Hamdu Shaka, aliwataka madiwani kuhakikisha wanapata, kuvitumia na kusimamia vitabu vya mipango mikakati minne ya wilaya vitakavyowasaidia kupiga hatua katika maendeleo wilayani humo.

Shaka alisema mpango mkakati ukiwamo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi hasa ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine ukitumika vizuri, utasaidia kupunguza migogoro hiyo kwa kiasi kikubwa.





# TAKUKURU yanusa rushwa fedha za halmashauri

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU) Mkoa wa Singida imebaini kuwapo kwa mianya ya rushwa katika baadhi ya halmashauri ikiwamo ya Mkalama kwa kukusanya michango kutoka kwa wananchi, kutumika kabla ya kuingizwa kwenye akaunti za vijiji.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Mzalendo Widege, akitoa taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi cha Januari - Machi 2023, alisema katika uchunguzi aliofanya wamebaini fedha za michango zinatumika kabla ya kuingizwa kwenye akaunti ya vijiji, baadhi ya wananchi hawapewi stakabadhi.

Aidha, alisema fedha zinatumika kinyume na madhumuni ya mchango, wenyeviti wa vitongoji na watendaji wa vijiji wanatumia fedha kwa matumizi binafsi.

Widege alisema wamebaini mianya ya rushwa katika usimamizi wa fedha za miradi ya maji chini ya kamati za maji za jumuiya za watumia maji ambapo wajumbe wa bodi wanajilipa posho kubwa, hakuna mwongozo wa viwango vya posho na mishahara na ukaguzi wa mahesabu haufanyiki.

Widege akizungumzia uendeshaji wa masoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni alisema wamebaini hakuna sheria ndogo za halmashauri zinazosimamia uendeshaji wa masoko, kuna usimamizi hafifu wa soko kupelekea vizimba kuwa wazi na wafanyabiashara wachache kulipa kodi.

Alitaja mambo mengine waliyoyabaini kuwa ni matumizi hayafuati taratibu, mfano ununuzi wa umeme na malipo ya mhudumu, baadhi ya mapato hayaingizwi katika mfumo wa mapato, kama mapato yatokanayo na maji na choo, rejesta ya wafanyabiashara hazihuishwi na kuna malalamiko ya mpango wa uboreshaji wa soko. Akizungumzia kuhusu uendeshaji na usimamizi wa vyama vya walimu Manispaa ya Singida, alisema wamebaini walimu wanakatwa makato ya CWT bila ridhaa yao na bila kujaza fomu TUF 15, ukinzani wa maslahi, mjumbe wa chama kuhusika katika kupitisha nakala pale mwanachama anapotaka kujitoa.

Alitaja mambo mengine waliyoyabaini ni kuwepo kwa mkataba wa uwakala baina ya Manispaa ya Singida na chama chenye wanachama wengi ambayo haijapitiwa kwa muda mrefu (kuhuishwa),mwajiri kukata fedha ya uwakala kwa wanachama na kuwasilisha CWT bila kuwa na akaunti maalumu.

Widege alisema taasisi hiyo imefuatilia utekelezaji wa miradi 28 ya Sh.bilioni tatu katika sekta za elimu na barabara ambayo inajumuisha miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19 na serikali.

Aliitaja miradi hiyo na thamani yake kuwa ni miradi ya elimu saba yenye thamani ya Sh. milioni 305, miradi ya barabara mitatu yenye thamani ya Sh. milioni 742.7, miradi ya afya 11 ya Sh. bilioni 2.03.

Alisema ufuatiliaji mwingine uliokaguliwa ulikuwa ni matumizi ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Singida, Manyoni na Ikungi kwa ajili ya makundi maalumu (wanawake, vijana na watu wenye ulemavu) na Sh.milioni 422.3 zilitengwa.

# Watumishi Mahakama waagizwa kuhamisha taarifa kidijitali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JAJI Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Ibrahim Juma ameagiza watumishi wa Mahakama kuhamishia taarifa zote kidijitali, kwamba wasihamie Dodoma na nyaraka kwenye karatasi.

Aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Mahakama ya Tanzania uliofanyika jijini hapa.

Alisema hivi sasa suala la teknolojia ni muhimu sana katika utendaji kazi, hivyo kila mtumishi ana wajibu wa kujifunza matumizi ya TEHAMA ili kurahisisha utendaji kazi na wanapohamia wasimamie na makaratasi.

"Mnapohamia hakikisheni kila kitu kinahifadhiwa kwenye teknolojia, nyaraka nyingine zitawekwa katika kumbukumbu ya nyaraka ya taifa,"alisema.

Alisema kila mmoja anapaswa kuweka jitihada katika suala zima la elimu ya TEHAMA ili inapofika kwenye utoaji huduma kwa jamii inakuwa rahisi kwake kufanya kazi kwa kutenda haki.

Mbali na hilo Prof. Juma aliwataka viongozi wa Mahakama kujenga utaratibu wa kutoa mrejesho wa vikao kwa watumishi wao ili wajue nini kinaendelea endapo kuna mabadiliko yoyote.

Alisema wanapaswa kuacha tabia ya ubinafsi wa kukaa kimya mpaka wasubiri kikao cha baraza la wafanyakazi ndipo waanze kuongea na wafanyakazi wao kuhusu masuala ya kiutendaji.

Aidha alisema ni wajibu wa kila mtu kufanya kazi kama timu, ufanisi na uwajibikaji utakomfanya kila mmoja kwa nafasi yake kutambua majukumu na mipaka ya uwajibikaji wake.

"Sheria inawapa nguvu, fanyeni kazi kwa kufuata miongozo, hakuna neno linalonivunja moyo kama ninapoambiwa naomba maelekezo yako, jambo unalotakiwa kusoma na kulielewa, na baadae ulifanyie utekelezaji lakini hakuna mtu mwenye muda huo."

"Maendeleo ya nchi yanakosekana kwa kukosa jitihada, ni wepesi kusambaza taarifa kuliko kuisoma na kuielewa kwa ufasaha, kila mtumishi ajenge tabia ya kujitafutia elimu, jitihada binafsi ndizo zitakazo kupambanua na wengine, hii siyo karne ya kulalamika ni ya kutatua matatizo," alisema Prof. Juma.

Pia, alisisitiza umuhimu wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA, ili kwenda sambamba kidijitali kwa kuhakikisha taarifa zote muhimu zinapatikana kwa wakati, kupitia mifumo (website) ili kuleta huduma bora kwa wananchi na kuwesha upatikanaji wa taarifa muhimu kwa wakati.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja Uhusiano wa Airtel, Jackson Mmbando kuhusu Rauter ya Intanet inayoweza kuunganisha watu zaidi ya 32 kwa wakati mmoja, alipotembelea maonyesho ya wadau wa mawasiliano katika viwanja vya bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# 'Wanachama ushirika changamkieni fursa za mafunzo'

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WANAUSHIRIKA mkoani Dodoma wameshauriwa kutumia fursa za mafunzo yanayotolewa katika jukwaa la ushirika ili kujiongezea maarifa na uwezo ya kuendesha na kusimamia kwa ufanisi shughuli za vyama vyao.

Akifungua jukwaa hilo jana, Mrajisi Msaidizi wa Mkoa wa Dodoma, Octavian Bidyanguze, alisema pamoja na mambo mengine jukwaa hilo lina malengo ya kuwaongezea ujuzi wa masuala ya ushirika.

Mrajis Msaidizi huyo alisema jukwaa hilo linatekeleza kazi ya msingi wa ushirika kimataifa wa elimu na mafunzo.

"Niwaombe wanaushirika mtumie fursa hii ya mafunzo kutoka kwa wakufunzi na wataalamu wetu leo ili mpeleke ujuzi mtakaopata hapa kwa wanaushirika wengine katika vyama vyetu vya ushirika," alisisitiza.

Mratibu wa Kanda ya Kati wa Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU), Bahati Rukiko aliwakumbusha wanaushirika kuwa na ushirikiano baina ya vyama ili kuendeleza na kuimarisha ushirika.

Alisema ushirikiano huo utasaidia kukuza masoko, kubadilishana uzoefu, kuongeza ubunifu na kujenga mahusiano baina ya vyama.

Mratibu alisema vyama vinapotekeleza dhana ya ushirika vinapata fursa ya kutatua kero za wanaushirika ndani ya ushirika.

"Kwa mfano chama kimoja kuwa na uzalishaji mkubwa wa mazao bila masoko ya kutosha wakati chama kingine kikiwa na uwezo wa uchakataji wa mazao vishirikiane ili kuongeza thamani kuongeza wigo wa masoko,"alisema.

Aliongeza kuwa ushirikiano baina ya vyama utasaidia vyama vya ushirika vitasaidia kukuza vyama vidogo na vile vinavyoanza na kuvipa uwezo wa kukua na zaidi na hatimaye kuwa na vyama imara zaidi vyenye msaada kwa wanaushirika.





# Dk. Mwinyi akutana na viongozi wa ACT-Wazalendo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amekutana na wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Chama cha ACT-Wazalendo, akiwemo Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zitto Kabwe, Mwenyekiti, Juma Duni Haji, Makamu Mwenyekiti Zanzibar, Othman Masoud Othman.

Dk Mwinyi alikutana na viongozi hao Ikulu Zanzibar, kujadiliana na kukubaliana hatua za kuchukua kukamilisha mchakato wa mageuzi ya kisheria yanayopaswa kufanyika Zanzibar ili kuimarisha haki, umoja na mshikamano.

Katika mazungumzo hayo, viongozi hao wa ACT-Wazalendo walimhakikishia Dk Mwinyi, utayari wao wa kuharakisha mazungumzo ya vyama vikuu vya kisiasa nchini ambayo yatasababisha utekelezaji wa mapendekezo ya kikosi kazi cha Zanzibar kuhusu mageuzi ya kisiasa, kiutawala na masuala ya uchaguzi. Kiongozi Mkuu wa chama hicho, Zito Kabwe, alisema tayari wamewasilisha majina ya timu ya majadiliano ya watu sita kutoka ACT-Wazalendo kwa Rais wa Zanzibar itakayoongozwa na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman ambae pia ni Makamu Mwenyekiti wa chama hicho.

Mwenyekiti wa chama hicho, Juma Duni Haji alimkabidhi taarifa rasmi ya ACT-Wazalendo kuhusu ukiukwaji wa haki za binadamu Zanzibar wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Katibu wa Habari, Uenezi, Mawasiliano na Umma ACT-Wazalendo, Salum Bimani alisema chama kinaunga mkono hatua ya viongozi hao kukutana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ikiwa ni utekelezaji wa azimio la kamati kuu na kamati ya uongozi taifa.

Hivyo aliahidi kutoa ushirikiano kuhakikisha mchakato huo unatekelezwa kwa maslahi ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla.

Bimani alisema: "Ni matumaini yetu kuwa kila mwenye kuitakia mema Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ataunga mkono hatua hii na tunatoa wito kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kujitokeza hadharani kuonesha kumuunga mkono Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar ambae pia nia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi".

# Dk. Mwinyi mgeni rasmi Jukwaa la Asasi za Kiraia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi leo anatarajia kufungua mkutano wa pili wa kitaifa wa Jukwaa la Asasi za Kiraia visiwani Zanzibar (ZANGUF), asasi za kiraia 250 kutoka Zanzibar na Tanzania Bara zitashiriki.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mkutano huo Mwenyekiti wa ZANGUF, Hassan Khamis Juma, alisema lengo la mkutano huo ni kujenga uelewa kwa asasi za kiraia, kuimarisha utawala bora hasa katika uwazi na uwajibikaji na kuweka mikakati itakayosaidia mipango na vipaumbele vya kitaifa.

Alisema lengo lingine ni kuainisha matatizo zinazoikabili sekta ya asasi za kiraia na kutafuta njia ya kupunguza au kuondosha na kuungana pamoja baina ya asasi za kiraia na serikali.

Alisema mada mbalimbali zitawasishwa na kujadiliwa katika mkutano huo wa siku mbili, ikiwemo mageuzi ya kisheria, umuhimu wa asasi za kiraia katika serikali, kufanya mageuzi ya kisheria ili kukuza utawala bora, uwajibikaji na uwazi.

"Ushirikiano utajengeka zaidi kwa kutekeleza mpango wa serikali ambao umejikita kuimarisha uchumi wa buluu, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali za nchi"alisema.

Aidha alisema mkutano wa kwanza uliofanyika mwaka jana umeleta mafanikio ikiwa mabadiliko ya sera na sheria na kutolea mfano Sheria ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar ya Mwaka 2006 na kupatikana kwa sheria mpya ya mwaka 2022.

Alisema asasi za kiraia bado zinaendelea kufanya masuala ya utetezi ili sheria, sera na miongozo mbalimbali iliyopitwa na wakati wanaifanyia kazi.

Katibu wa ZANGOF, Mahfoudh Haji alisema ikitokezea kuna asasi ambayo imegundulika kuwa zinaunga mkono vitendo vya mapenzi ya jinsia moja zitatengwa.




Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (katikati) akishuhudia wakati Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Philip Besiimire (kulia) na Kiongozi wa Ujumbe wa serikali ya Marekani kutoka USAID, Kate Somvongsiri (kushoto), wakionyesha nyaraka baada ya Vodacom Tanzania Foundation na USAID, kutiliana saini wa mkataba wenye thamani ya dola za kimarekani milioni 5 (zaidi ya Sh. bilioni 11.8) jijini Dar es Salaam jana, ili kuiunga mkono serikali katika utekelezaji wa mfumo wa m-mama nchini. M-mama inapatikana kupitia namba ya bure 115 mitandao yote bara na visiwani ambapo zaidi ya akinamama 21,800 na watoto wachanga wamesafirishwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake watakiwa kuchangamkia bil.39/- za corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Sabiha Filfil Thani, amewataka wanawake kuchangamkia Sh.bilioni 39 za ugonjwa wa corona zilizotengwa kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani, wakati akiwasilisha maoni ya kamati hiyo katika Bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

Alisema Serikali ya Zanzibar imetenga fedha nyingi ambazo zimelenga kuwakomboa wajasiriamali na hali ngumu ya maisha lakini bado fedha hizo hazijatumika kikamilifu.

Alisema fedha hizo zimegawika katika makundi mbalimbali ikiwemo fedha kwa ajili ya wakulima wa mazao ya baharini ikiwemo kilimo cha mwani, ufugaji wa matango bahari, kaa na samaki.

"Juhudi kubwa zimefanywa kwa upande wa wajasiriamali wakulima wa mwani ambapo jumla ya boti 500 zimetengenezwa kwa ajili ya kuwawezesha wakulima kulima mwani katika kina kirefu cha maji"alisema.

Aidha alitaja juhudi zinazochukuliwa na serikali kwa sasa katika kujenga mazingira mazuri ya wakulima wa mwani ambao asilimia 80 ni wanawake ni pamoja na kujenga viwanda viwili vya kusarifu zao hilo na kuliongezea thamani sokoni.

Kwa upande wa mazao ya baharini alisema, tayari mabwawa 100 yametengenezwa kwa ajili ya wafugaji wa matango bahari kufuga katika mbinu za kisasa, huku kituo cha kuzalisha vifaranga kimeanza kazi.

Naye Waziri wa Maendeleo ya Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema Bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji imewalenga wanawake kujikomboa kutoka katika utegemezi hadi kuwa wazalishaji wakubwa wa bidhaa mbalimbali zitakazowawezesha kuingia sokoni kwa mafanikio makubwa.

Alisema kuanzishwa kwa vituo vya kukuza wajasiriamali maarifa na mbinu za uzalishaji wa bidhaa ni sehemu ya ushahidi tosha wa mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwakomboa wajasiriamali kuingia katika uchumi wenye tija.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24



MHE. NAPE MOSES NNAUYE (MB.)
WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIOA YA HABARI



MHE. MHANDISI KUNDO ANDREA MATHEW (MB.)
NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIOA YA HABARI



NDG. MOHAMMED KHAMIS ABDULLA,
KATIBU MKUU WA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIOA YA HABARI



MHE. MHANDISI KUNDO ANDREA MATHEW (MB.)
NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIOA YA HABARI

JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**A. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2022/23.

Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

Naomba hotuba yangu yote iingie kwenye kumbukumbu za Bunge kama ilivyowasilishwa mezani.

**Mheshimiwa Spika,**
Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika Mkutano huu wa kumi na moja wa Bunge la kumi na mbili.

**Mheshimiwa Spika,**
Nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake madhubuti katika kipindi hiki cha zaidi ya miaka miwili ambacho kimekuwa na maendeleo na uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Kipekee nichukue nafasi hii kumshukuru sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Isdori Mpango kwa maelekezo yake na miongozo yake ambayo kwakweli imesaidia sana katika kutimiza majukumu yetu Wizarani.

Naomba pia kumshukuru sana Mhe Waziri Mkuu wa Tanzania Mhe. Majaliwa Kassim Majaliwa kwa usimamizi wake kwetu,miongozo yake na maelekezo yake kwetu ambayo yamekuwa chachu ya ufanyaji kazi wetu.

Wizara inatambua matarajio makubwa waliyonayo wananchi ya kufikishiwa huduma za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kama ilivyofafanuliwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

**Mheshimiwa Spika,**
Nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge lako Tukufu kwa weledi, busara na hekima kubwa. Ninapenda kulishukuru Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano wao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu Wizara.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa upekee niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mheshimiwa Seleman Moshi Kakoso Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela Mbunge wa Jimbo la Same Mashariki na Wajumbe wote wa Kamati.

Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia majukumu yanayosimamiwa na Wizara. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika Hotuba hii. Nawaahidi mimi na wenzangu Wizarani, hatutawaangusha.

**Mheshimiwa Spika,**
Kwa masikitiko makubwa natoa pole kwako Mheshimiwa Spika na Wabunge wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Hayati Mussa Hassan Mussa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Amani, Zanzibar kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Nitoe pole pia kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki wa marehemu, pamoja na wananchi wa Jimbo la Amani kwa kuondokewa na mpendwa wetu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika,

Wizara inasimamia Taasisi tisa, ambazo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania; Shirika la Mawasiliano Tanzania; Shirika la Posta Tanzania; Shirika la Utangazaji Tanzania; Kampuni ya Magazeti ya Serikali; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote; Tume ya TEHAMA; Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Hotuba hii itaelezea kwa ufupi masuala yanayotekelezwa na Wizara pamoja na Taasisi inazosimamia.

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara iliidhinishiwa kutumia kiasi cha Shilingi bilioni 282.06, Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 26.3 ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 255.8 ziliidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Hata hivyo hadi kufikia mwezi Aprili, 2023 Wizara imepokea na kutumia jumla ya Shilingi bilioni 125.1. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 12.8 sawa na asilimia 48.7 ya fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 112.3 sawa na asilimia 43.9 ya fedha za mendeleo.

**Ukusanyaji wa Mapato**
**Mheshimiwa Spika,** kufikia tarehe 30 Aprili, 2023 Wizara imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 24.9 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, tozo kuongeza salio, mauzo ya picha za Viongozi Wakuu wa nchi, machapisho na ada ya mwaka ya magazeti.

Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imeendelea na upangaji wa masafa kwa Huduma za Mawasiliano, ambapo mnada wa masafa ulifanyika tarehe 11 Oktoba, 2022 kwenye bendi za 700 MHz, 2300 MHz, 2600 MHz na 3500 MHz ambayo yanatumika kwa ajili ya mawasiliano ya simu na intaneti katika kuwezesha huduma za 4G na 5G nchini.

Makampuni manne ya ndani yalifanikiwa kushinda zabuni kwa mauzo ya Dola za Marekani milioni 187.5. Hadi mwezi Aprili, 2023 asilimia 75 ya fedha hizi kiasi cha Dola za Marekani milioni 140.6 zimeshalipwa na kuingia Mfuko Mkuu wa Serikali.

**B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

Katika Mwaka wa 2022/2023 Wizara imetekeleza masuala yafuatayo:-

**Sekta ya Habari**

**Mheshimiwa Spika,**
Katika Mwaka wa Fedha 2022/23 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imefanya masuala yafuatayo:-

i. Mapitio ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 ambapo muswada wa marekebisho ya Sheria hiyo umesomwa Bungeni kwa mara ya kwanza mwezi Februari, 2023;

ii. Imeratibu Mikutano 13 ya Msemaji Mkuu wa Serikali na kuainisha mafanikio ya Serikali na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali. Jumla ya Vipindi 25 vya Televisheni vinavyohusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo viliandaliwa na kurushwa hewani. Tumefanikiwa kujenga Studio ya muda Jijini Dodoma kwa ajili ya kuzalisha vipindi vya Kitaifa na kimkakati.

Pia, kumekuwepo na ongezeko la vituo 5 vya utangazaji wa maudhui ya ndani ya kulipia ambayo imetoa fursa ya ajira kwa wasanii wa ndani kwenye maudhui yenye muktadha wa filamu, michezo ya kuigiza na tamthilia.

TBC imeboresha maudhi yanayorushwa kwenye redio, televisheni na mitandao ya kijamii. Ubunifu wa kimaudhui na uwasilishaji umeongeza mvuto kwa vyombo vya Habari vya TBC. Aidha, TBC ilifanikiwa kununua HAKI za kutangaza michuano ya Kombe la FIFA la Dunia. Ambapo jumla ya michezo 28 (ilirushwa TBC ONE) na michezo yote 64 (ilirushwa TBC Taifa na TBC Online). Uanzishwaji wa kurusha taarifa ya Habari kwa Kiingereza umeanza mwezi Novemba, 2022 na hivyo kupanua wigo wa Habari zinazotolewa na Shirika hilo.

iii. Vituo vya kurusha matangazo ya redio vimeongezeka kutoka 210 mwaka 2022 hadi kufikia vituo 215 Mwezi Aprili, 2023 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga vimeongezeka kutoka 56 mwaka 2022 na kufikia vituo 65 Mwezi Aprili, 2023.

Serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya matumizi ya teknolojia za Utangazaji hasa maudhui mtandaoni

ambayo pia yamechangia kuongeza ajira kwa vijana. Katika kuimarisha usimamizi katika Sekta ya Habari Wizara kupitia TCRA na Idara ya Habari – Maelezo imetoa jumla ya leseni mpya 20 za magazeti zimetolewa na leseni 18 za maudhui ya mtandao zimetolewa;

iv. Serikali imeendelea kuboresha huduma za Utangazaji hususani wa redio jamii katika maeneo ya vijijini. Serikali kupitia UCSAF imeendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya kurushia matangazo na studio za redio ya Taifa katika maeneo ya kimkakati na mipakani. Maeneo mbalimbali Miradi hii imekamilika kama vile Mlimba Mkoani Morogoro, NgoroNgoro Mkoani Arusha, Ludewa Mkoani Njombe, Ruangwa Mkoani Lindi, Ngara Mkoani Kagera.

**Mheshimiwa Spika,**

v. Kupitia magazeti ya Dily News, Habari Leo na Habari Mtandao Kampuni ya Magazeti ya Serikali Tanzania (TSN) imeendelea kutekeleza mpango wake mahsusi "Editorial Transformational Plan" kwa kuandika Habari za kina za uchambuzi.

vi. Mradi wa kufunga mtambo mpya wa kisasa wa uchapaji unaendelea ambapo ununuzi na upokeaji wa mtambo wa magazeti utafungwa;

**Sekta ya Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika,**

Kulingana na Kitabu cha Hali ya Uchumi wa Taifa, Sekta ya Habari na Mawasiliano imekua kwa kasi ya asilimia 9.1 mwaka 2020. Ukuaji huu unathibitishwa na ongezeko la upatikanaji na matumizi ya huduma za mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,**

Takwimu zinaonyesha laini za simu zilizosajiliwa kuongezeka kutoka milioni 55.7 Mwezi Aprili, 2022 hadi kufikia milioni 62.3 Mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 11.8.

Watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka Milioni 29.9 Mwezi Aprili, 2022 hadi kufikia Milioni 33.1 Mwezi Aprili, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 10.7. Takwimu hizi zinaashiria hali ya ukuaji wa Sekta.

Katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imetekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 ambapo rasimu imekamilika na kuwasilishwa kwa wadau;

ii. Utungwaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Kanuni zake ikiwemo mchakato wa uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

iii. Maboresho ya Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kwa ajili ya kuweka mazingira wezeshi ambayo yamezingatia maslahi mapana ya wananchi pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji;

iv. Katika Sekta ya Mawasiliano tumefanikiwa kuandaa mkakati wa Sekta ya Mawasiliano wa kuimarisha ushiriki wa nchi Kikanda na Kimataifa ambapo Tanzania imefanikiwa kupata nafasi katika Baraza la Umoja wa Mawasiliano Afrika na Umoja wa Mawasiliano Duniani;

v. Kufanikiwa kutekeleza Mfumo wa Anuani za Makazi Nchini kupitia Mradi wa Anuani za Makazi na Postikodi. Aidha, Mfumo wa Anuani za Makazi umeweza kuunganisha Taasisi za Umma kama vile Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuboresha taarifa za wamiliki wa viwanja, pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa kuboresha taarifa za walipa kodi.

vi. Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Intaneti ambapo jumla ya laini za simu 997 zilizokuwa zikitumika kwenye mawasiliano ya ulaghai wa mawasiliano ya simu za Kimataifa zilisitizwa matumizi yake;

vii. Usimamizi wa zoezi la usajili na uhakiki wa laini za simu Nchini ambapo hadi tarehe 30 Aprili, 2023 laini za simu zinazotumika kwenye Mitandao ya simu zimefikia milioni 63,317,168 zimesajiliwa kwa alama za vidole;

viii. TCRA imetoa jumla ya leseni 26 kwa watoa huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi;

ix. Ujenzi wa Jengo la Umoja wa Posta Afrika unaojengwa kwa ubia na TCRA ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 98

x. Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limekabidhiwa rasmi jukumu la kutekeleza Mradi wa Mkongo wa Taifa (NICTBB), na Kituo cha Taifa cha Kutunzia Data (NIDC);

xi. Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limeendelea kufanya maboresho na usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji kodi kwa njia ya kielektroniki ujulikanao kama e-RCS (Electronic Revenue Collection Sysytem);

xii. Mikataba ya upelekaji huduma za mawasiliano vijijini imesainiwa ambapo jumla ya minara 758 kwa ajili ya kupeleka huduma za mawasiliano itajengwa na jumla ya Minara 304 itaongezewa nguvu chini hafla ambayo ilishuhudiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Pia, jumla ya minara 42 katika Shehia 38 imekamilika na kuzinduliwa Zanzibar hafla ambayo ilishuhudiwa na Mheshimiwa Rais, wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri. Ufikishaji wa huduma za mawasiliano vijijini ikiwemo maeneo ya Kimakati kama Bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Julius Nyerere , Msomera- Handeni.

**Eneo la TEHAMA**

**Mheshimiwa Spika;**

Katika eneo hili Wizara imetekeleza yafuatayo;

i). Kusimamia na kuratibu utungwaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ya mwaka 2022 Aidha, Wizara imekamilisha kuandaa Kanuni za kuwezesha utekelezaji wa Sheria hii;

ii). Kuwezesha kujenga uwezo wataalamu 500 wa Jeshi la Polisi kwenye nyanja ya usalama mtandao.

iii). Kusimamia maendeleo ya ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

vi). Kukamilisha taratibu za kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya upembuzi yakinifu wa Kituo cha Kuhifadhi Data Zanzibar

v). Kukamilisha upembuzi yakinifu wa kubaini maeneo yenye changamoto ya mawasiliano ili kuwezesha ujenzi wa minara 758 ambayo mikataba ya ujenzi wake imesainiwa tarehe 13 Mei, 2023 na kushuhudiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**Mheshimiwa Spika,**

Maeneo mengine ambayo Wizara imeendelea kuyafanyia kazi kwa kipaumbele ni pamoja na;

i). Ukamilishaji wa Mpango Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali (Digital Economy Framework 2023-2033),

ii). Kuhuisha ununuzi wa Mkondo wa Mawasiliano ya Serikali (Extension of Government Internet Bandwidth) wenye kasi ya 5Gbps,

iii). Kufanikiwa kuandaa Daftari la huduma za Serikali kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi (Government Service Directory) ambapo taarifa zimekusanywa kutoka Taasisi 57 za Serikali.

iv). Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA, ambapo shughuli zifuatazo zimetekelezwa: kukamilika kwa usanifu wa Kituo cha Kampuni changa za TEHAMA cha Kanda ya Dar es Salaam na kutengeneza mfumo jumuishi utakaowezesha kuwa na taarifa za wabunifu, kampuni za TEHAMA, wawekezaji katika huduma na bidhaa za ubunifu katika TEHAMA, Vituo atamizi vya TEHAMA na Vituo vya uendelezaji bunifu za kidijitali.

**Mheshimiwa Spika,**

Utekelezaji wa Majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Wizara umeainishwa katika Ukurasa wa 34 hadi 59 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**C. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

**Makadirio ya Mapato ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara inakadiria kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 150.7 ambazo zitatokana na mauzo ya huduma za;

i). Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano,

ii). Tozo itokanayo na kuongeza salio la simu,

iii). Usajili wa Magazeti na ada ya mwaka ya Magazeti,

iv). Vitambulisho vya Waandishi wa Habari na machapisho ya picha, mabango na majarida.

**MALENGO YA BAJETI YA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA FEDHA 2023/2024**

**Eneo la Habari**

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Sekta ya Habari Wizara itatekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Kufanya mapitio ya Sera ya Habari na Utangazaji ya Mwaka,2003 ilikuendana na mabadiliko katika Sekta ya Habari,

(ii) Kuratibu utungwaji wa Sheria ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC),

(iii) Kujenga studio maalum kwa ajili ya vipindi vya moja kwa moja vya redio na televisheni,

(iv) Kuanzisha redio ya Afrika itakayotangaza kwa lugha ya kiswahili kwa lengo la kuendeleza matumizi ya kiswahili na kujenga umoja wa Afrika.

(v) Kuendelea kusimamia Sekta ya Habari kwa kutoa Leseni

(vi) Kuhamasisha vyombo vya habari vya nje katika kutangaza Tanzania

(vii) Kuendelea kujenga na kufunga miundombinu ya utangazaji katika Wilaya tisa kati ya Wilaya 21 ambazo hazina usikivu au zina usikivu hafifu;

(viii) Kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu ya TBC Jijini Dodoma;

(ix) Ununuzi wa mitambo na vifaa vya utangazaji vya redio, Televisheni na Mitandao ya kijamii kwa lengo la kuunganisha studio tano za Mikocheni, Zanzibar, Barabara ya Nyerere, Dodoma na Arusha,

(x) Kununua gari moja ya kurushia matangazo ya Televisheni mbashara,

(xi) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya kiwanda cha uchapaji na kufunga mitambo ya kisasa ya uchapaji,

(xii) Kuanza taratibu za ujenzi wa Kituo cha Habari ambacho kitajumuisha Chaneli ya Televisheni ya Serikali, studio ya kuzalisha maudhui, vyumba vya mikutano, mifumo ya kufuatilia habari zinazotokea duniani na kutoa fursa kwa waandishi wa habari kufanya kazi pamoja.

**Eneo la Mawasiliano**

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kufanya mapitio ya Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu ya Mwaka 1997 na kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003;
ii. Kuratibu uimarishaji wa upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu na Posta kote nchini
iii. Kuanzisha utaratibu mahususi wa kugawa masafa kwa ajili ya redio za utangazaji kidijitali;
iv. Kuratibu utungwaji wa Sheria ya kuimarisha matumizi na kuhakikisha uendelevu wa mfumo wa Anwani za Makazi;
v. Kuratibu uanzishwaji wa anga la Juu nchini ikiwemo kufanya maandalizi ya kurusha Satelite katika kuwezesha urahisi na unaafuu katika upatikanaji wa huduma za Mawasiliano Nchini.
vi. Kuandaa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano,
vii. Kusimamia utekelezaji wa biashara Mtandao (e-Commerce).
viii. kuratibu uanzishwaji wa maghala maalum ya kuhifadhi bidhaa, huduma ya ugomboaji na ushuru wa forodha ili kuwezesha biashara mtandao
ix. Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Brodibandi wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy);
x. Kuratibu utekelezaji wa mradi wa miundombinu ya mawasiliano ya simu, redio na televisheni vijijini.
xi). Ukamilishaji wa shughuli za ujenzi wa Kilometa 1,742 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa Kuratibu ujenzi wa Kilomita 60 za mkongo wa mawasiliano kupitia Ziwa Tanganyika kuunganisha Tanzania na Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Kuratibu ujenzi wa Kilometa mpya 1,600 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kufikisha huduma ya Mkongo kwenye Wilaya 14,na Kujenga Mikongo ya kuunganisha watumiaji ambao ni Taasisi 50 kwenye maeneo ya uwekezaji, huduma za afya na elimu ili kuharakisha Taifa kushiriki katika uchumi wa kidijitali.

**Eneo la TEHAMA**

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA nchini, Wizara inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Kuhuisha Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016 na kuandaa Mkakati wa utekelezaji,
ii). Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa matumizi ya Teknolojia zinazoibukia(emerging technologies) kama vile Artificial Intelligence, Robotics, IoT, ili kuiwezesha nchi kufikia Mapinduzi ya Nne ya viwanda(4th Industrial Revolution)
ii. Kuratibu na kuwezesha matumizi ya Mfumo wa Mikutano ya Video (video conferencing) katika ngazi ya Wizara, Mikoa 26 na Halmashauri 185 nchini;
iii. Kufanya tathmini ya uanzishwaji wa 'smart cities' katika mikoa ya Dodoma, Arusha na Mbeya;
iv. Kuendelea na uratibu wa uendelezaji wa Mifumo ya Kitaifa nchini;
v. Kuandaa Mkakati wa kuboresha matumizi ya Tafiti za TEHAMA,
vi. Kuendelea kuboresha Usimamizi na uanzishwaji wa Kampuni Changa za TEHAMA kwa kuboresha mazingira ya Kisera, Kisheria na Kikanuni na kuweka miongozo stahiki.
vii. Kuanzisha vituo vitano vya kanda vya kusaidia kukuza Taaluma na ubunifu wa TEHAMA;
viii. Kuunganisha Taasisi za Serikali kwenye mtandao mmoja (GoVNET);
ix. Kuwezesha usimikaji wa Vituo vya Huduma Pamoja nchini;
x. Kujenga maabara tatu kwa ajili ya kufufua vifaa vya TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza; na
xi. Kujenga uwezo kwa wataalam wa TEHAMA 500 Serikalini katika maeneo yenye wataalamu haba ikiwemo Artificial Intelligence,Big Data Analytics,Machine Learning, Augumented Reality.
xii. Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Zanzibar na kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Data Dodoma; pamoja na kusimamia uanzishwaji wa Vyuo viwili vya TEHAMA vya Nala na Kigoma,

**Mheshimiwa Spika,**

Serikali ya Awamu ya sita imedhamiria kuwezesha nchi kuelekea katika uchumi wa kidijitali hususani kuhimiza mfumo wa kufanya biashara bila fedha taslimu (cashless economy) ambao unaowezeshwa na kuendeshwa na TEHAMA.

Ili kufanikisha haya kwenye Sekta zote za Uchumi na Kijamii, Wizara imepanga kufanya mabadiliko na maboresho makubwa kwenye Sekta ili kuendana na mageuzi haya ikiwemo kuharakisha ujenzi, uendelezaji na usimamiaji miundombinu ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Vilevile, Wizara itafanya mapinduzi kwenye Taasisi za Sekta kwa lengo la kuimarisha mashirikiano na Sekta binafsi, kuendeleza tafiti na ubunifu kwenye masuala ya TEHAMA ikiwemo uanzishwaji na uendelezaji wa kampuni changa (startups), kuwezesha Sekta nyingine kuelekea kwenye mapinduzi haya ya kidijitali; na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari nchini.

Aidha, Wizara yangu itahakikisha Uchumi wa Kidijitali unawekewa mazingira bora ya kiudhibiti na kiuwekezaji ikiwemo kuandaa sera, miongozo na taratibu za kulinda maadili ya Kitanzania na kuhakikisha usalama mtandaoni.

**Eneo la Usalama Mtandao**

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara inatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kufanya tathmini ya Mkakati wa Kitaifa wa Usalama Mtandaoni 2018 - 2023 na kuandaa na kutekeleza Mkakati mpya wa 2023 - 2028;
(ii) Kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Elimu kwa Umma kuhusu Usalama Mtandao 2021/22 - 2025/26;
(iii) Kusimamia ukamilishwaji na utekelezaji wa usimamizi wa Miundombinu Muhimu ya TEHAMA (Critical ICT Infrastructures);
(iv) Kuimarisha muundo wa kiutawala na kiusimamizi wa ulinzi dhidi ya uhalifu wa mtandao nchini; na
(v) Kuimarisha uwezo wa wakaguzi wa ndani kufanya ukaguzi wa mifumo.

**Mheshimiwa Spika,**

Ili kujenga uwezo wa Wizara kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Shughuli zifuatazo zitatekelezwa:-

i) Kuendeleza watalaam wa ndani na nje ya Sekta kwa kutoa mafunzo ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya TEHAMA na elimu ya matumizi ya teknolojia mpya zinazoibukia kwenye sekta nyinginezo;
ii) Kuwajengea uwezo Waandishi wa Habari na Wahariri wa Vyombo vya Habari;
iii) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa kununua vitendea kazi; na
iv) Kuelimisha umma juu ya teknolojia mpya za kidijitali, kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi salama na yenye tija ya TEHAMA huku wakilinda haki za watoto, wanawake, makundi maalum na vijana.

**Mheshimiwa Spika,**

Shughuli zitakazotekelezwa na Taasisi tisa zinazosimamiwa na Wizara zimeainishwa kwenye ukurasa Na. 74 hadi 82 wa Kitabu cha Hotuba ya Bajeti.

**SHUKRANI**

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa moyo wa dhati ninapenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kunisaidia kutekeleza majukumu yangu katika Wizara hii. Kipekee niwashukuru Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew (Mb.), Naibu Waziri; Mohammed Khamis Abdulla, Katibu Mkuu na Selestine Gervas Kakele, Naibu Katibu Mkuu.

Aidha, naishukuru Menejimenti ya Wizara, Wenyeviti wa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zinazosimamiwa na Wizara; Viongozi wa Taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara na Taasisi kwa kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha kuwa Wizara yetu inakuwa chachu ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kipekee nichukue fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo ambao Serikali imekuwa ikishirikiana nao katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Sekta za Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Baadhi ya washirika hao ni: Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano; Shirika la Umoja wa Posta Duniani; Shirika la Umoja wa Posta Afrika; Benki ya Dunia kupitia dirisha la Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa.

**Mheshimiwa Spika,**

Ningependa pia kuzishukuru Jumuiya za Kikanda na Kimataifa za Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Ulaya kwa ushirikiano katika masuala ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu Sekta hii. Kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara yangu itaendelea kuimarisha ushirikiano na Washirika wa Maendeleo na wadau wengine ili kuhakikisha kuwa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inachangia katika kutimiza Dira ya Taifa ya kufikia Uchumi wa Kati wa Juu ifikapo Mwaka 2025.

Mwisho sio kwa umuhimu naomba kuwashukuru kwa dhati wananchi wenzangu wa Jimbo la Mtama kuendelea kuniamini na wakati mwingine kunivumilia wakati natimiza majukumu yangu. Nina wapenda na kuwathamini sana, tuendelee kuchapa kazi pamoja.

Siwezi sahau upendo, uvumilivu na kunitia moyo kwa familia yangu wakiongozwa na binti yangu Jayla, wanangu Jaydan na Jayson na mama yao mke wangu Rhobi. Nawashukuru kwa upendo wao, kunivumilia hasa ninapokosekana kwa muda na namna wanavyonitia moyo katika kutimiza kazi zangu.

**MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA KWA WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24**

**Mheshimiwa Spika,**

Katika Mwaka wa Fedha 2023/24, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 212,457,625,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

i) Kiasi cha Shilingi 30,503,685,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi 18,522,155,000 ni za Mishahara na Shilingi 11,981,530,000 ni za Matumizi Mengineyo; na

ii) Kiasi cha Shilingi 181,953,940,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo Shilingi 146,777,440,000 ni Fedha za Ndani na Shilingi 35,176,500,000 ni Fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika,**

Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni **http://www.mawasiliano.go.tz** na pia kwa kutumia QR Code ambayo imesambazwa kwenu.

***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.




Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohammed Mchengerwa (wa pili kushoto) akiwa katika pikipiki zilizokabidhiwa na Benki ya CRDB kwa Kituo cha Polisi cha Utalii na Diplomasia jijini Arusha juzi, kwa ajili ya kusaidia katika doria na kuimarisha ulinzi na usalama kwa watalii. Wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kushoto), Mkuu wa Wilaya Arusha, Felician Mtahengerwa (kulia), na Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchakato uanzishaji benki ya ushirika waanza

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

UONGOZI wa vyama vya ushirika nchini umeanza kutekeleza azma ya ukusanyaji wa Sh. bilioni 15 kwa ajili ya uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ya Taifa, itakayosaidia kukuza uchumi na kufanikisha uhakika wa mikopo yenye riba nafuu kwa wanachama wake.

Akizungumza jana jijini Arusha kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Arusha, Naibu Mrajisi Udhibiti Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Collins Nyakunga alisema kuwa uanzishwaji wa benki hiyo, utawanufaisha wanachama wake ikiwamo kuondokana na matatizo ya upatikanaji wa fedha.

Alisema kuwa wanataka kusajili Benki ya Taifa ya Ushirika ambapo mtaji wa Sh.bilioni 15 unahitajika, kwa ajili ya kuanzisha benki hiyo, huku wanachama wakiendelea na uchangiaji wa fedha hizo kwa ajili ya uanzishwaji wake.

Aliongeza kuwa hivi sasa wana Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro, ambapo hadi kufikia Machi 30 mwaka huu walikuwa na mtaji wa Sh.bilioni 5.2 uliokusanywa hadi sasa kutoka kwa wanachama na wadau.

"Mikakati yetu ni kuibadilisha Benki ya Ushirika ya Mkoa wa Kilimanjaro kuwa Benki ya Taifa ya Ushirika (NCBT) na bado tunaendelea na ukusanyaji wa fedha na tunatarajia hadi ifikapo Juni mwaka huu, tuwe na benki hiyo,"alisema Nyakunga.

Alisema nchini Kenya tayari wana benki za ushirika na nchi zingine mbalimbali na kupitia benki hizo zimefanikiwa kwa kiwango kikubwa kiuchumi, ambapo uwepo wa benki hiyo utasaidia katika masuala ya riba na kupata mikopo kwa wakati na haraka.

Mwenyekiti wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Arusha, Shedrack Issangya, alisema kuwa mchakato wa kuanzishwa kwa Benki ya Taifa ya Ushirika unaendelea hivyo ni wajibu wa kila chama cha msingi kununua hisa kwenye benki hiyo na kuendelea kuwahamasisha wanachama wengine kununua hisa ili waweze kumiliki benki yao.

Aidha, aliviomba vyama vyote vya msingi vinavyolima mazao mchanganyiko vilivyopo Mkoa wa Arusha, Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara kuanza kulima kilimo cha kisasa, kwa kutumia pembejeo bora za kilimo na kutumia mbinu za kisasa, ili kuongeza tija kwenye kilimo badala ya kuendelea kulima kilimo cha mazoea.

Issangya alisema kuwa, mikakati waliyonayo ni kuwaandaa vijana kujiunga na vyama vya ushirika na kuhakikisha mali na miradi ya chama hicho inanufaisha jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

# Matukio ya ukatili 89 yarekodiwa miezi mitatu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

JESHI la Polisi limerekodi kesi 89 za ukatili wa kijinsia katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu.

Kamanda wa Polisi mkoani Manyara Kamishna Msaidizi (ACP), George Katabazi, alitoa takwimu hizo wakati akizungumza na wazee wa Wilaya ya Babati.

Kwa mujibu wa Katabazi, kesi 52 za ukatili zimeripotiwa katika Wilaya ya Babati, kati ya hizo nyingi ni za ubakaji na ulawiti, huku waathirika wakuu wakiwa ni watoto wenye umri miaka miwili mpaka minane.

Aidha, alisema lengo la kuwaita wazee hao na kujadiliana nao kwa pamoja ni kutaka kuzuia na kutanzua uhalifu.

"Nimekuja kusisitiza ushirikiano katika kuzuia uhalifu na sehemu yenye usalama ndio kunapatikana maendeleo,"alisema Katabazi

Alisema bila ushirikiano, Jeshi la Polisi haliwezi kukomesha uhalifu ikiwemo ukatili wa kijinsia kwa watoto.

Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Babati, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi, Raphael Mwandu, aliwaomba wazee kuwatumia vijana wao kufanya ulinzi shirikishi ili kukomesha uhalifu.

Katika mkutano huo, mzee Felix Kivuyo, alisema suala la ulawiti limekuwa janga la kitaifa, hivyo wazee waache kukubali kumalizana kienyeji kwa kupeana mbuzi au kondoo.

Kivuyo alisema watu wanaobaka na kulawitiwa wasipewe wanasheria wa serikali wa kuwatetea.

Kwa upande wake, Thomas Samo, alisema wapelelezi wengi hawapelelezi kesi kwa weledi bali wanapelekeza kwa rungu.

Hivi karibuni, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alisema matukio ya ukatili dhidi ya watoto yaliongoza mwaka jana, ambapo ubakaji yalikuwa 6,335 na ulawiti matukio 1,557.

Mikoa iliyoongoza ni Arusha (728), Mbeya (710), Kinondoni (681), Tanga (607) na Mwanza (595).

# Wafugaji wanne mbaroni tuhuma kujeruhi wakulima

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WAFUGAJI wanne wa jamii ya kimasai wanashikiliwa kwa tuhuma za kuhusika katika mapigano ya wafugaji na wakulima yaliyosababisha wakulima watatu kujeruhiwa na nyumba moja kuteketezwa kwa moto.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe, alithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao.

Mapigano hayo yalitokea juzi katika mashamba ya Lelugunya yaliyoko Kijiji cha Gitu, Kata ya Kibirashi.

"Nitatoa maelezo baada ya kupata taarifa kamili lakini waliokamatwa hadi sasa ni watu wanne kuhusiana na tukio hilo na majeruhi wote watatu wamelazwa kwenye Kituo cha Afya cha Songer," alisisitiza Mwaibambe.

Baadhi ya mashuhuda akiwemo Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Gitu, Omar Mbota, alisema mapigano hayo yalizuka jana majira ya saa 8:10 mchana baada ya wafugaji hao kuvamia mashamba ya wakulima na kuwashambulia kwa silaha za kijadi.

Akielezea tukio hilo kwa njia ya simu ya kiganjani, alisema muda huo walipata taarifa za mapigano hayo kwa njia ya simu na kwamba baada ya kufika eneo la tukio walikuta watu watatu wakiwa wamejeruhiwa.

Alieleza kuwa walioshambuliwa kwenye mapigano hayo ni Mawazo Mihinza, Anthon Melkion na Ismail Lesikali na kwamba katika tukio hilo nyumba moja ya Petro Laizer ilichomwa moto.

"Baada ya hapo tulichukua hatua za kuwakimbiza polisi kwa ajiri ya kuokoa maisha yao huku wengine tuliendelea na msako wa kuwatafuta waharifu hao ambao kwa wakati huo walitoweka baada ya kufanya shambulio hilo" alieleza.

Hata hivyo alidai kuwa kutokana na msako unaoendelea hivi sasa wameshakamatwa watu watatu wanaohisiwa kuhusika na tukio hilo huku wengine wakiendelea kutafutwa.

Wakielezea zaidi tukio hilo wakazi wa Kijiji cha Gitu walidai kuwa wafugaji hao walifanya uvamizi huo wakitumia mbwa kwa ajiri ya kuwadhibiti wanaokimbia kujinusuru.

Mmoja wa wananchi hao,Haji Juma, aliiomba serikali kuona umuhimu wa kutafuta ufumbuzi wa kukomesha matukio hayo ambayo mara nyingi licha ya wakulima kujeruhiwa lakini pia husababisha vifo na mali.

Peter Oleika, alisikitishwa na namna suala hilo linavyo shughulikiwa kwa kuwa mara zote halipewi kipaumbele linapomuathiri mkulima tofauti na akishambuliwa mfugaji wa jamii ya kimasai.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Tamthilia ya 'Siri Binti Kasri' ilivyotikisa ITV

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni hekaheka, patashika nguo kuchanika nchini Tanzania pale muda wa tamthilia ya 'Tausi' ulipokaribia. Kwanza kabisa siku ya onyesho hilo lililokuwa likionyeshwa kituo cha televisheni ya ITV, kinamama watapika chakula mapema.

Watoto wataoga mapema. Muda ukifika, akinamama na watoto wao kutoka kwenye nyumba hata kumi, watakwenda kwenye nyumba ambayo ina televisheni kuangalia mchezo huo.

Nikukumbushe tu hiyo ni mwishoni kabisa mwa miaka ya 90 hadi 2000 mwanzoni. Kama ni kijana wa sasa na hujui ilivyokuwa ni kwamba kipindi hicho si Watanzania wengi waliokuwa na televisheni. Ni nyumba 10 kwa moja. Sehemu nyingine unaweza ukakuta kijiji kizima mwenye TV ni mmoja tu.

Na wale ambao waliokuwa na televisheni kwenye mambo kama ya tamthilia walikuwa hawapendi kuangalia peke yao, hivyo kuwaalika majirani. Hii ipo hata kwenye soka. Ni aghalabu sana mtu kuangalia peke yake.

Hata hivyo kuna baadhi walizitumia kama fimbo ya kuwachapia wenzao, kwani kuna wakati wakikuwa wanawafukuza, wanawasimanga, ili mradi tu.

Akinamama watakaribishwa kwenye makochi, wengine watatandikiwa mikeka, na watoto watakaa chini, huku wakipewa maonyo ya kuacha utundu na kutopiga kelele.

Mara utasikika wimbo wa 'Tausi', ulipigwa kwenye miaka ya 1960 na mwanamuziki Mkenya sehemu za Mombasa, Fundi Konde.

'Tausi ndege wangu. Ndege wangu wa fahari. Ndege umekwisha mali, sasa wataka nini? Wapita watu wawili, walioleta ulamali, sasa tuko mbalimbali.'

Wimbo huo ulichukuliwa na ukawa ndiyo wimbo wa kufungulia tamthilia hiyo, ambayo ilitokea kuwa maarufu mno nchini na isiyosahaulika kamwe.

Yapo mambo mbalimbali yaliyoifanya tamthilia hiyo ambayo ilitungwa, kuchezwa na kutolewa nchini Kenya, huku wasanii wote walioigiza wakiwa ni Wakenya.

Kwanza kabisa ni kwamba, pamoja na kwamba TV ndiyo zilikuwa zinaingia nchini na si watu wengi waliokuwa nazo, lakini televisheni binafsi kubwa nchini ITV ilikuwa haina muda mrefu toka kuanzishwa.

Pili ni kwamba hakukuwa na filamu na tamthilia za kiswahili wakati huo kwa sababu hakukuwa na televisheni, hivyo ITV kwa kuwapenda waangaliaji wake waliwatafutia tamthilia iliyochezwa kwa lugha ya kiswahili na watu ambao wakati mwingine kuna uingiliano wa kitamaduni na ni majirani, yaani Wakenya.



Rehema



Rukia

Tatu ni kwamba huo ndiyo ulikuwa wakati ambao Watanzania ndiyo walikuwa wanaanza kuangalia televisheni, hivyo bado walikuwa na hamu ya kuangalia vitu mbalimbali.

Wengi wanawakumbuka wasanii waliocheza tamthilia hiyo ambao baadhi yao sasa ni marehemu.

Hao ni Maua, Ondieki, Rhoda, Mponda, mzee Kasri, Ashina, Kibibi, Sango, Zinzi, Dk. Kurya, Bi. Popo, Master Sugu, Sikitu, Jesca Brown, Dama, Rehema na Chokoraa damu, kina, Lindi, Vita, Joto.

Yupo pia jamaa mmoja anaitwa Mjuba, halafu kukawa na mganga wa kienyeji aliyeitwa Kalumanzira.



Sitti.



Lindi

Athali ya tamthilia hii kukawa na watu wakajiita Chokoraa, akiwa wababe wakaitwa Wajuba, na waganga wa kieneji wakaanza kuitwa Kalumanzira

Msanii ambaye tutamzungumzia kidogo hapa ni Ashina Kibibi, ambaye aliigiza kama Siti Binti Kasri.

Huyu ndiye mtunzi wa tamthilia hiyo. Ndiyo alikuwa kama staa wa mchezo mzima. Wakati yeye akicheza kama Siti Binti Kasri, akawapa majina yake ya ukweli baadhi ya washiriki, mmoja akawa Ashina na mwingine Kibibi.

Kwa mujibu wake mwenyewe, ni kwamba majina hayo yote ni ya bibi zake, upande wa baba na upande wa mama. Hakutaka kuweka jina la baba mbele.

Alikuja nchini Tanzania mwanzoni mwa miaka ya 2000, bila kujua kama yeye ni staa nchini.

Alifikia eneo la uswahilini Mwananyamala kwa mjomba wake. Pamoja na kuwa ni Mkenya wa Mombasa, Ashina pia alikuwa na asili ya Tanga. Baadhi ya ndugu zake walikuwa ni Watanzania wa Tanga. Kilichotokea hakuamini. Watu walianza kumfananisha.

Walipoulizia uliziwa na ndugu zake, waliambiwa kuwa ni yeye. Kilichotokea ni kwamba watu walikuwa wanaitaka kutoka pande mbalimbali. Nyumba ikazingirwa. Kila mtu si wakubwa si watoto walitaka kumuona Siti Binti Kasri laivu. Wakavunja ukuta wa nyumba.

Gazeti na Guardian na Nipashe ndiyo walikuwa ya kwanza kuandika ujio wake. Yakatoa picha zake japo awali yeye hakutaka hivyo kwa madai ulikuwa ni ujio binafsi na wa kifamilia. Ndipo alipojigundua kuwa yeye ni staa sana nchini Tanzania na hakupaswa kuja kama alivyokuja. Utambulisho wake ulimsaidia kupata mikataba ya kufanya maonyesho nchini. Alikuja na kufanya hivyo mara kadhaa. Safari zilizofuata alikuwa akifikia Embassy Hotel na kwenda kwa ndugu zake kusalimia tu na kuondoka na si kukaa huko huko kama mwanzo.

Kwa bahati mbaya sana, Ashina alifariki mwaka 2005 kwa kujinyonga mwenyewe kwenye mti wa mwembe kwao Mombasa nchini Kenya.

Tamthilia ya 'Tausi' kwa kiasi kikubwa ndiyo iliyosababisha msukumo wa tasnia ya sanaa ya maigizo nchini, kwani lilianzishwa kundi la Kaole ambalo lilikusanya wasanii mbalimbali wachanga, ambao baadaye wakawa wasanii wakubwa kama kila Ray Kigosi, marehemu Steven Kanumba, Mzee Jengua na wengine wengi ambao wote walibebwa na televisheni ya ITV.

Hapo ndipo baadaye walitoka na kwenda kucheza filamu, maarufu kama bongo movie. Hivyo ukiona filamu za bongo movie, tamthilia mbalimbali za kiswahili nchini, msingi wake haswa ni tamthilia ya 'Tausi' chini ya televisheni ya ITV ambayo imechangia sana kuwepo kwa tasnia hizo nchini Tanzania.

**Tuma meseji 0716 350534**



HABARI KIMATAIFA

# Mapigano yaendelea kurindima Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

MASHAMBULIZI makali ya anga yameendelea kutikisa maeneo ya kusini mwa mji mkuu wa Sudan, Khartoum huku mapigano yakipamba moto karibu na kambi ya kijeshi.

Viongozi wawili wanaowania madaraka, na kusababisha machafuko yanayoendelea Sudani ni kiongozi wa kijeshi Abdel al-Burhan na kamanda wa kikosi cha RSF Mohamed Dagalo, huku mapigano yakiingia mwezi wa pili sasa.

Kwa mujibu wa mashuhuda, mashambulizi hayo ya anga ya jeshi dhidi ya wanamgambo wa Msaada wa Haraka (RSF), yalisikika katika makazi kadhaa ya vitongoji kusini mwa Khartoum, pamoja na karibu na kambi ya Taiba, huku kikosi cha akiba cha polisi kikishirikiana na jeshi kupambana na wanamgambo wa RSF.Ilielezwa kuwa jeshi limekuwa likitumia zaidi mashambulizi ya anga na silaha nzito wakati likijaribu kuwarejesha nyuma wanamgambo wa RSF ambao wamesambaa viunga vya maeneo ya Khartoum na miji inayopakana ya Bahri na Omdorman.

Vurugu pia ziliripotiwa magharibi mwa Khartoum katika eneo la Nyala, moja ya miji mikubwa ya Sudan na mji mkuu wa jimbo la Darfur Kusini.

Mmoja wa mashuhuda alidai kwamba milio ya silaha nzito ikiwa ni pamoja na mizinga ilisikika kwa mara ya kwanza tangu makubaliano ya kusitisha mapigano.

Ilibainishwa kuwa magenge yenye silaha yameanza uporaji katika mji mwingine mkubwa wa El Obeid, ambao ni kitovu cha biashara katika jimbo la Kordofan Kaskazini.

Shirika la mpango wa chakula la Umoja la Mataifa, lilisema kuwa linazidisha operesheni zake angalau katika majimbo sita ya Sudan ili kuwasaidia watu takriabni milioni tano walio hatarini.

Umoja wa Mataifa (UN) kupitia ofisa anayehusika na misaada ya kiutu Martin Griffiths, alilaani ukiukaji mkubwa wa makubaliano ya pande zinazozozana nchini humo wiki iliyopita na kutoa rai ya kuruhusu misaada inayohitajika kwa haraka.

Griffiths ambaye anaongoza juhudi za kiutu za UN, alikaribisha makubaliano ya Mei 12 yaliyotiwa saini mjini Jeddah na pande mbili katika mzozo huo zilizoapa kujizuia kushambulia misafara ya misaada.

"Kutiwa saini kwa hati hiyo, pamoja na ulinzi wake wa matakwa ya kibinadamu, inasisitiza kwamba hakupaswi kuwepo na mashambulizi dhidi ya wafanyakazi wa kibinadamu au majengo. Siku mbili zilizopita kulikuwa na shambulio kwenye ofisi ya Mpango wa Chakula Duniani huko Khartoum," alisema.

Kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, hadi sasa mapigano hayo yamesababisha vifo vya watu zaidi ya 1,000, zaidi ya watu 840,000 wamekimbia makazi ndani ya Sudan na wengine zaidi ya 200,000 wamekimbilia nchi za jirani.

**DW**



Wafungwa wakitoka katika gereza lililoko katika mji mkuu wa Zimbabwe, Harare, baada ya msamaha wa rais. **PICHA: AFP.**

# Maelfu ya wafungwa waachiwa huru Zimbabwe

**HARARE,** ZIMBABWE

KIASI cha theluthi moja ya wafungwa wote nchini Zimbabwe wameachiliwa huru kutokana na msamaha wa rais wa taifa hilo, alioutoa miezi michache kabla ya uchaguzi mkuu.

Kwa mujibu wa taasisi ya Huduma za Wafungwa na Magereza nchini Zimbabwe (ZPCS), wafungwa 4,270, wengi wao wanaume, waliachiliwa huru jana, na kwamba kitendo hicho ni kama ishara ya kiungwana ya rais wa taifa hilo.

"Tungependa kutoa wito kwa jamii kwa ujumla kuwathamini na kuwajali wafungwa walioachiliwa, na wale waliodhulumiwa wanahimizwa kusamehe," ilisema ZPCS.

Ilielezwa kuwa hatua hiyo inapunguza msongamano wa watu katika jela zaidi ya 50 nchini humo, ambazo zina uwezo wa kuhudumia watu takribani 17,000 lakini zimekuwa zikiwashikilia zaidi ya mahabusu 22,000 kabla ya msamaha huo kutolewa.

Hata hivyo, msemaji wa ZPCS Meya Khanyezi aliliambia shirika la habari la AFP, kwamba sababu ya kuachiliwa kwa wafungwa hao sio kupunguza msongamano, bali ilikuwa ni nia nzuri tu ya rais.

Pia ilibainishwa kuwa msamaha huo umetolewa kwa makundi mbalimbali ya wafungwa wakiwemo wale waliotumikia angalau robo tatu ya vifungo vyao, au moja ya kumi ikiwa walihukumiwa vifungo vya zaidi ya miaka 60.

Aidha, ilielezwa kuwa msamaha huo haukuwahusishi wahalifu wanaotumikia vifungo kwa wizi, uhaini na kuvuruga amani kwa umma na makosa ya usalama. Hata hivyo, wale walioachiliwa wataweza kupiga kura katika uchaguzi wa rais na wabunge ambao unatarajiwa kufanyika Agosti, mwaka huu ingawa tarehe ya uchaguzi bado haijatangazwa.

"Rais alishatoa msamaha kama huo katika kilele cha janga la Covid-19 mwaka 2020 kwa nia ya kupunguza kuenea kwa virusi katika mahabusu," alisema.

**VOA**

# G7 kujadili uimarishaji vikwazo dhidi ya Russia

**HIROSHIMA,** JAPAN

VIONGOZI wa nchi saba zilizostawi zaidi kiviwanda, G7, wamekutana nchini Japan kwa mkutano wa kilele wa jumuiya hiyo, ikiwa ni pamoja na kujadili uimarishaji wa vikwazo dhidi ya Russia na ulinzi dhidi ya shurutisho la kiuchumi kutoka China.

Viongozi hao kutoka Marekani, Japan, Ujerumani, Ufaransa, Uingereza, Italia na Canada walikutana jana, na lengo la mkutano huo utakaofanyika siku tatu ni kuonyesha umoja dhidi ya Russia na China.

Mshauri wa Usalama wa Kitaifa wa Marekani, Jake Sullivan, alisema Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, anatarajiwa kushiriki katika mkutano huo kwa njia ya video na kwamba majadiliano kuhusu hali ya uwanja wa vita yanatarajiwa.

Sullivan alisema suala la kuimarishwa kwa vikwazo dhidi ya Russia linapaswa pia kushughulikiwa na nchi wanachama, na kwamba viongozi hao watajadili pia kuhusu kukabiliana na msukosuko wa vikwazo, ambao unamruhusu Rais wa Russia Vladimir Putin kuendelea kufadhili juhudi zake za vita.

Pia ilielezwa kuwa nchi za G7 zitalazimika kukubaliana juu ya jinsi ya kujilinda kutokana na uhujumu wa kiuchumi unaowezekana kutoka kwa Beijing.

Kwa mujibu wa Sullivan, viongozi wa G7 wanapaswa kukemea shurutisho hilo la kiuchumi na kujitahidi kuondokana na tofauti za kupita Atlantiki kuhusu msimamo wa kupitisha China.

Alisema kwa nchi nyingi za Ulaya, hasa Ufaransa na Ujerumani, kuondoa hatari haimaanishi kukata uhusiano na China, ambayo ni mojawapo ya soko kubwa duniani, akieleza kuwa sio kundi la G7 linaloipinga China, badala yake kinachohitajika ni ujumbe chanya wa ushirikiano.

Nchi nane, zikiwemo India na Brazil, pia zimealikwa kushiriki mkutano huo, lengo likiwa ni kuwakusanya baadhi ya viongozi ili kupinga vita vya Ukraine na matarajio ya Beijing.

**RFI**

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-9

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Kundi la saba linaanguka kwa wale wanaoitwa 'licensed to kill'. Wauaji wenye vibali, leseni za kuua. Hawa huwa ni waajiriwa wa mamlaka za nchi kama yeye mwenyewe Eddy Kamal. Na hufanya hivyo kwa manufaa ya nchi. Hata wakiua hawakamatwi. Wako tayari kufanya chochote kile kwa ajili ya kuilinda na kuitetea nchi ili wananchi waishi kwa amani na utulivu, dhidi ya watu waovu, wasaliti, ambao wapo tayari kuiuza hata nchi au kuhujumu mali za nchi na miundombinu, ikiwemo kutaka kuwafanya wananchi wasiishi kwa amani na utulivu.

Wanyongaji wao wamewekwa kwenye kundi la mwisho wakiitwa 'the hungers.' Tofauti na watu wanavyowafikiria hawa ni watu wema sana, na wanafanya kazi hiyo ikiwa kwao ni ajira rasmi kama zingine. Kazi yao kubwa ni kuwanyonga wahalifu wote waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa. Hawa wakati mwingine hufanya ibada pamoja na watu wanaotarajia kuwanyonga.


Eddy alitabasamu baada ya kumalizia kupitia tabia ya wauaji, mauaji na makundi yao. Sasa hapo kazi yake ikawa moja tu. Ni kutafuta mauaji ya mwanamama Tessy yako kwenye kundi gani? Lipi? na inawezekana kuwa mauaji hayo yapo kwenye kundi moja tu la mauaji au mawili?

Atakapopata ni aina gani ndipo atakapoanza upelelezi na wapi pa kuanzia kutokana na kuona kabisa maelekezo ya mauaji inawezekana ikawa ni watu wa aina fulani. Ni akina nani na kwa nini, hilo litajulikana baadaye.

Yeye baada ya hapo kazi yake kuu itakuwa ni kunusa taarifa, habari na kuzifanyia kazi kwa kutumia njia yoyote ile ya kuhadaa, au kufanya chochote kile ili mradi kupatikana kwa wahusika wakiwa hai au wamekufa, na pia kufahamu sababu ilyosababisha yote hayo, na kisha kuishauri mamlaka kuchukua hatua.

Kwanza kabisa aliangalia aina ya kifo cha Tessy, na kurudi kwenye aina nane ya mauaji au wauaji, akaona inaangulia kwenye maeneo mawili.

Kundi la nne, la tano Tessy aliuawa na kukatwatakatwa viungo vyake vikatumbulizwa kwenye kiroba na kwenda kutupwa kama uchafu.




**"Hata kama wangemkaba mpaka kufa, isingewezekana wao kuanza kazi ya kumkatakata viungo." Alijiambia.**

Hii inaonyesha kuwa mwanamama huyo ameawa kwa mateso. Muuaji alimuua taratibu kwa kutenganisha viungo kimoa baada ya kingine.

Hakudhani kama alimuua kwanza na kuanza kumkatakata. Wauaji wa aina hii ya nne, ni kwamba walikuwa na hasira kali dhidi ya mhusika, hivyo muuaji au wauaji walitaka kumuonyesha kuwa wao ni nani na wanaweza kumfanya lolote, pia kuona wanakufa kwa mateso, ili kiondoa hasira ya kile kilicho moyoni mwao. Marehemu alimfanya nini muuaji au wauaji? Eddy alijiuliza.

Akayaweka mauaji hayo pia kwenye kundi la tano la aina ya wauaji, ambao wana msongo wa mawazo 'stress.'

Inawezekana ni mtu huyo alikuwa na maumivu ya mapenzi, kama inavyosema kuwa ni watu ambao hufikia kuona kila mmoja ni adui yake, anaweza kumuua mtu yoyote hata watoto wake na yeye kujimaliza.

Eddy Kamal aliamua kuanza kucheza humo, na aliondokana kabisa na wazo la maaskari kwa kuwakamata waokota chupa za plastiki na wazoa taka kuwa wamefanya mauaji hayo.

"Hawa kama watakuwa wametumika labda ni kuubeba tu mzigo, lakini haingii akilini watu wa aina hii kumuua mtu, wakamkatakata na kuweka kwenye kiroba.

Mara nyingi hawa huwa ni vibaka tu, wenye njaa, ambao kazi yao ingekuwa rahisi tu, kumwamuru mwanadada huyo awape vitu alivyokuwa navyo kwa kumtishia silaha yoyote hata msumari tu akawapa, wakaondoka taratibu, bila ya kujipa kazi nyingine yoyote ya ziada." Alijisema mwenyewe ofisini hapo.

Athari kubwa ambao 'mateja' ambao wangeweza kumpa marehemu Tessy ni kumkaba shingo tu na si kumuua.

"Hata kama wangemkaba mpaka kufa, isingewezekana wao kuanza kazi ya kumkatakata viungo." Alijiambia.

Hapo tayari alikuwa ameshaiweka kazi yake vizuri kabla hata hajaanza. Kilichobakia sasa ni kuanza utekelezaji. Nao ni upelelelezi.

**************************

Kazi ya upelelezi ni nini? Ni kukusanya ushahidi ambao wakati mwingine unaweza kuwa mgumu kama huu wa mauaji ya Tessy.

Upelelezi mara nyingi huwa mgumu kutokana na mazingira ya tukio lenyewe, pengine mwili umeokotwa, umekutwa, umetupwa majini, umeungua au kuaribiwa vibaya, kwa hali kama hii inahitajika kupima vinasaba, kupima alama za vidole, kupima mifupa hata kama mwili ulikuwa umeshafukiwa, kupata baadhi ya vifaa alivyotumia marehemu ikiwemo hata mavazi.

Vipimo vyote vitakavyopimwa hulenga kubaini mambo mengi ila baadhi ni sababu ya kifo chake, kimesababishwa na nani au nini kama sumu, panga, risasi, na sehemu ambayo tukio lilipotokea.

Kuchunguza eneo jirani lilipotokea tukio, hapa mpelelezi ni lazima ave uhusika wa kirafiki, kijasusi na kuweza kuwafanya majirani, jamaa na mashuhuda wakuone ni mtu wa kawaida ambaye hawamtilii mashaka na kuogopa kusema kile walichohuhudia.

Mpelelezi pia anakuwa kujua marehemu alikuwa anadhamiria nini siku chache kabla ya kuuawa, alikuwa vipi na uhusiano na wenzake nyumbani kama vile mahusiano ya ndoa, kazini, lakini pia hata kwenye mitandao ya kijamii ambako huenda alivurugwa.

Pia kwa miaka ya sasa anatakiwa kuwa mjuzi wa kupekua na kutumia vifaa vya kisasa ambavyo ambavyo vikitumia ipasavyo anaweza kupata chanzo cha mauaji, kama kompyuta, simu, vinasa sauti, magari, CCTV, flash na vingine vingi.

Kwa dunia ya sasa anatakiwa kuwa mbobezi na mtundu wa mambo ya IT kama alivyo Eddy Makal, kwani anaweza kuichezea kompyuta atakavyo.

Alichojifunza kwenye dunia ya sasa wahalifu nao wamekuwa na tabia ya kujiongeza sana, hivyo ukiwa mzembe watakutesa mno.

Dunia tuliyopo uhalifu kwa njia ya mitandao hauepukiki isitoshe mifumo yote ya kifedha, huduma za msingi za kijamii, mawasiliano, ulinzi na usalama, utawala na uendeshaji wakati mwingine mpaka vyombo vya usafiri, vyote viko chini ya mawasiliano na mitandao, hivyo wakati wahalifu wanataka kufanya ubaya, watu wa usalama wanaweka mambo sawa na wakati mwingine kuwakamata.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# KAZE: UBORA WA WACHEZAJI SIRI YA MAFANIKIO YANGA CAF

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema mafanikio makubwa ambayo timu hiyo imeyapata msimu huu yametokana na kuwa na idadi kubwa ya wachezaji wenye viwango vikubwa na vinavyofanana.

Akizungumza mara baada ya kuwasili Dar es Salaam jana wakitokea Afrika Kusini katika mechi ya marudiano ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Marumo Gallants ambapo walipata ushindi wa jumla wa mabao 4-1, Kaze, alisema msimu huu wamepata mafanikio kutokana na wachezaji wote kujituma kila walipopata nafasi.

Kaze alisema wachezaji wamepambana katika kila mechi na walikuwa wakionyesha ushirikiano ndani na nje ya uwanja.

“Yanga msimu huu tunajivunia kuwa na kikosi cha wachezaji wenye viwango vikubwa na vinavyofanana, akikosa huyu atacheza huyu, ukiwapumzisha hawa watacheza wengine na wanaoingia viwango vya havipishani na waliopumzika. Ndiyo maana utaona tunacheza vizuri kila mechi. Wachezaji wote waliosajiliwa wamechangia kwa asilimia kubwa na si kikundi tu fulani cha wachezaji na wengine wamekaa tu,” alisema Kaze.

Kocha huyo raia wa Burundi alisema kama wangekuwa na sehemu tu ya wachezaji ambao ndiyo wana viwango vikubwa kuliko wengine, wasingefanya vyema katika mashindano ya kimataifa na kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

“Tumechukua ubingwa wa Tanzania Bara, tuko nusu fainali ya Kombe la FA na fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika, hii inaonyesha tuna wachezaji bora na wanaofanana na kukaribiana sana viwango, vinginevyo hali isingekuwa hivi. Angalia mfano tumecheza Jumatano iliyopita Afrika Kusini, tumesafiri, tumefika Dar, tutapanda ndege kwenda Dodoma, halafu tutasafiri tena kwa basi kwenda Singida ili tucheze nusu fainali.

Siku ya Jumapili tuna mechi ya fainali dhidi ya USM Alger, nakwambia kama una wachezaji hao hao unakwama, lakini kama kawaida sisi tutatumzisha baadhi ya wachezaji, tutachezesha wengine ambao uwezo wao ni sawa tu na waliopumzika,” alisema Kaze.

Yanga inatarajia kujiandaa kuwakaribisha USM Alger kutoka Algeria katika mechi ya kwanza ya fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Waalgeria hao wamesonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuwaondoa ASEC Mimosas kwa ushindi wa jumla wa mabao 2-0.



Mchezaji wa PSMC, Karim Abdul (kulia), akiwania mpira dhidi ya nyota wa JMK, Hassan Haji, katika mechi ya kirafiki iliyofanyika kwenye Uwanja vya Jakaya Kikwete, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Wanyenche apania Ladies Open*

**Na Shufaa Lyimo**

NAHODHA wa timu ya taifa ya gofu ya wanawake, Hawa Wanyenche, amesema amejiandaa kufanya vyema katika mashindano ya Ladies Open mwaka huu ambayo yatafanyika leo na kesho kwenye klabu ya Jeshi la Wananchi Lugalo, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti la Nipashe jana, Wanyenche, alisema shindano hilo linatarajiwa kuwa gumu na lenye upinzani mkubwa kutokana na washiriki wengi watakaoshiriki kujiandaa vizuri.

Wanyenche alisema wachezaji wengi wana viwango vizuri hivyo kila mmoja amejipanga kuonyesha ubora wake katika mashindano hayo.

“Kwa upande wangu nimejipanga vyema kuhakikisha tunapata ushindi ili tuzidi kuitangaza klabu yetu kupitia shindano hilo,” alisema Wanyenche.

Nyota huyo aliongeza amefanya mazoezi kwa muda mrefu anawataka Watanzania hasa wanawake wajitokeze kwa wingi kuangalia vipaji vitakavyoonyeshwa.

“Ninaomba wanawake waje kwa wingi kuangalia namna wanawake wanavyojua kucheza mchezo wa gofu, michezo inajenga afya,” nahodha huyo alisema.

Aliongeza lengo la shindano hilo ni kupata wachezaji watakaokwenda kushiriki mashindano ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika Novemba 11, mwaka huu nchini Rwanda.

Shindano hilo linalofanyika kwa mara ya tatu kwenye klabu hiyo linashirikisha wachezaji kutoka klabu mbalimbali za gofu nchini ambazo zimekidhi vigezo.

# Parimatch yazindua Chomoka na Boda

**Na Mwandishi Wetu**

ZIKIWA zimepita wiki chache za kufanya maboresho katika tovuti ya kubashiri na sasa tumewawezesha wateja kutumia huduma ya ‘kushare’ mkeka na marafiki, Kampuni ya Parimatch Tanzania imezindua kampeni mpya ya Chomoka na Boda, imeelezwa.

Ofisa Habari na Mawasiliano kwa Umma wa Parimatch Tanzania, Ismael Mohamed, alisema jana kwa sasa mashabiki watabashiri kwa kutumia intaneti kidogo yenye kasi kubwa wakati wa kuperuzi.

Alisema wameamua kutambulisha kampeni hiyo ili kuendelea kuwathamini wateja wao kwa kuwapa burudani na vitu vyenye faida.

“Tumeamua kuzindua rasmi kampeni yetu ya CHOMOKA NA BODA ambayo itawapa fursa wateja wetu na Watanzania kiujumla kujishindia bodaboda mpya na simu janja aina ya VIVO Y22,” alisema ofisa huyo.

Aliongeza kampeni hii ni mahususi kwa wateja wao wote wa Parimatch wenye akaunti na hata wateja wapya watakaojiunga katika kipindi hichi cha kuelekea kumalizika kwa ligi mbalimbali duniani.

“Katika kipindi cha kuanzia leo (jana) 19.06.2023, mteja wa Parimatch akifanya bashiri kwenye mchezo wowote kupitia www.parimatch.co.tz basi ataingia moja kwa moja katika droo wa kuwania bodaboda aina ya Hero Hunter 125cc na smartphone aina ya VIVO Y22 (Simu janja). Kila siku tutakuwa tunatoa simu moja na washindi watakuwa wanatangazwa kupitia kurasa zetu za kijamii na zawadi ya bodaboda itatolewa kwa wiki mara moja siku ya Ijumaa kupitia droo itakayoruka Mubashara ITV wiki husika.”

Aliongeza pamoja na hayo, katika promosheni hiyo, sehemu ya michezo ya TVBET, Live Casino, Casino New na michezo ya Virtual hairuhusiwi kushiriki katika promosheni hiyo.

Parimatch ndio kinara wa michezo ya kubashiri mtandaoni na imekuwa ikitoa ofa kubwa ya bonasi ya ukaribisho ya asilimia 100 hadi kufikia Sh. milioni moja kwa wateja wapya.

Mbali na soka, Parimatch iliyoanza kufanya kazi nchini mwaka 2019, pia hutoa mamia ya matukio kila siku kwenye tenisi, UFC, mpira wa kikapu, kriketi na baseball.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MANE ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United na Newcastle United zimeibuka kuwa timu zenye uwezekano mkubwa zaidi wa kumsajili fowadi wa Bayern Munich na Senegal, Sadio Mane, mwwnye umri wa miaka 31, kufuatia msimu mbaya wa kwanza nchini Ujerumani. (***Mail***)

### ORBAN AGOMBEWA EPL

CHELSEA, Manchester United, Tottenham na Fulham ni miongoni mwa klabu zinazomhitaji mshambuliaji wa Gent mwenye umri wa miaka 20 kutoka Nigeria, Gift Orban. (***Evening Standard***)

### RABIOT ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inakamilisha mipango yao ya uhamisho wa majira ya joto, huku kiungo wa kati wa Juventus Mfaransa, Adrien Rabiot, mwenye umri wa miaka 28 akirejea kwenye orodha yao walioteuliwa pamoja na mlinzi wa Napoli wa Korea Kusini Kim Min-jae (26). (***Mirror***)

### LIVERPOOL YASAKA MAJEMBE

PAMOJA na kiungo wa kati wa Brighton aliyeshinda Kombe la Dunia la Argentina, Alexis Mac Allister mwenye umri wa miaka 24, Liverpool wanamfuatilia kiungo wa kati wa Chelsea na England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24, huku kiungo wa kati wa Bayern Munich na Uholanzi, Ryan Gravenberch (21), akiwa ni mchezaji mwingine anayewindwa. (***Liverpool Echo***)

### KOKCKU KUTUA ENGLAND

LIVERPOOL pia inavutiwa na kiungo wa Feyenoord na Uturuki, Orkun Kokcu, mwenye umri wa miaka 2 kama mbadala wa Mac Allister na kiungo wa kati wa Dortmund, Jude Bellingham (19). (Footbal Transfers)

### GVARDIOL ATAKIWA CITY

MANCHESTER City imeonyesha nia ya kumsajili beki wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol, huku klabu hiyo ya Ujerumani ikitaka pauni milioni 85 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Mail)***

### LOFTUS-CHEEK SOKONI

KIUNGO wa kati wa Chelsea na England, Ruben Loftus-Cheek, mwenye umri wa miaka 27 anasakwa na AC Milan ambao wanatazamia kujijenga upya kufuatia kushindwa kwao dhidi ya Inter Milan katika nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulya. (***Fabrizio Romano on Twitter***)

### SLOT AKARIBIA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur imeanza mazungumzo ya kumteua kocha wa Feyenoord, Arne Slot, kama kocha wao mpya. (Football Insider)

### CHELSEA YAMNASA PAEZ

KIUNGO wa kati wa Ecuador, Kendry Paez, ameripotiwa kusajiliwa na Chelsea kwa ada ya pauni milioni 20 huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 16 pia akiivutia Manchester United. (El Canal del ***Futbol, via Mirror***)

### BRENTFORD NA TONEY

KLABU ya Brentford inatazamiwa kuanza mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa England, Ivan Toney, mwenye umri wa miaka 27 mwishoni mwa msimu huu licha ya kufungiwa kwa miezi nane kutojihusisha na soka kwa makosa ya kamari. (***Mail***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MOURINHO: SIFA ZOTE WANASTAHILI WACHEZAJI

**ROME,** Italia

**Asema ni furaha kubwa kucheza fainali nyingine Europa huku...**

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, amesema hana mpango wa kuwa gwiji katika klabu hiyo baada ya kuiongoza timu yake kutinga fainali ya pili mfululizo ya Ulaya kwa ushindi wa jumla wa 1-0 dhidi ya Bayer Leverkusen katika mechi ya nusu fainali ya pili ya Ligi ya Europa iliyochezwa juzi.

**Kocha huyo mwenye umri wa miaka 60, ambaye alishinda shindano hilo la daraja la pili la ngazi ya kla bu la Ulaya mwaka 2017 akiwa na Manchester Unit ed, aliiongoza Roma kutwaa taji la Ligi ya Europa Con ference msimu uliopita.**

"Malengo yangu sio kuashiria nafasi yangu katika vitabu vya historia ya Roma," alisema Mourinho akiambia Sky Sport.

"Inasaidia watoto hawa (wachezaji) kukua, kufikia mambo muhimu," alisema. "Pia inawasaidia mashabiki wa Roma, ambao wamenipa mengi tangu siku ya kwanza. Ni furaha kubwa kufika fainali nyingine.

"Vijana walijitoa kwa kila, mchezo huu ni matokeo ya kazi yetu, uzoefu, busara na kujua jinsi ya kusalia kwenye mechi. Ni timu ya ajabu."

Mourinho alitoa shukrani zake kwa mashabiki wa Roma kwa uungwaji mkono wao wa kipekee katika kipindi chote cha kampeni ya Ligi ya Europa, huku akiomba uungwaji mkono wao kuendelea huku timu ikijiandaa kurejea katika mechi ya nyumbani ya Serie A dhidi ya Salernitana itakayochezwa keshokutwa.

"Sijui kama naweza kuuliza chochote zaidi kutoka kwa mashabiki, lakini vijana hawa wanastahili kitu maalum."

Hata hivyo, nahodha wa Roma, Lorenzo Pellegrini, alisema sifa zote zinapaswa kuelekezwa kwa Mourinho kwa mafanikio ya timu hiyo.

"Yeye ni tofauti, anakufanya utambue umuhimu wa mechi. Tulikuja hapa na kila mtu anajua anachopaswa kufanya," alisema.

"Tunasoma, tunajipanga, tunatazama video. Hasa Ulaya, unaweza kuona kile ambacho kocha anaituletea. Mourinho ndiye muundaji wa molari yetu hii."

Roma wako katika nafasi ya sita kwenye Serie A wakiwa na pointi 59, pointi mbili nyuma ya AC Milan na sita dhidi ya Lazio katika nafasi ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,114,9
MECHI KALI
BOURNEMOUTH
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 5.12
X | 4.17
2 | 1.53
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# HENDERSON AMTAJA MILNER, FIRMINO

**LIVERPOOL,** England

NAHODHA wa Liverpool, Jordan Henderson, amekiri litakuwa pengo kubwa kuondoka kwa James Milner na Roberto Firmino.

Wawili hao, ambao usajili wao msimu wa joto wa 2015 ulitangulia na kuwasili kwa kocha sasa Jurgen Klopp kwa miezi michache, wamekuwa na jukumu muhimu katika mafanikio yao ya hivi karibuni ya klabu hiyo.

Wote wawili wataondoka mikataba yao itakapokamilika mwisho wa msimu huu na Henderson anaamini litakuwa pengo kubwa kwao.

Kuhusu mchango wa Milner, kiungo huyo wa kati wa England aliliambia Shirika la Habari la PA: "Thamani kubwa kwa timu.

"Nadhani kocha alisema kikamilifu kwa kuwa hatukuweza kupata chochote bila Millie. Ni mhusika mkuu na kiongozi mkubwa ndani ya timu.

"Hakika itakuwa ajabu kutomwona Liverpool msimu ujao, amekuwa wa ajabu tangu alipokuja klabuni.

Firmino, ambaye amerejea mazoezini wiki hii baada ya kukosa mechi sita kutokana na tatizo la misuli, anastahili kuaga kihisia katika mechi ya mwisho ya nyumbani ya Liverpool msimu huu dhidi ya Aston Villa.

# *Klopp afungiwa mechi mbili EPL*

**LONDON,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amefungiwa mechi mbili kwa kumkashifu mwamuzi, Paul Tierney.

Klopp amesimamishwa na kutozwa faini ya pauni 75,000 kufuatia maoni yake kwa vyombo vya habari baada ya mechi dhidi ya Tottenham Hotspur iliyochezwa Aprili 30, mwaka huu, Chama cha Soka cha England (FA), kilisema jana.

Baada ya ushindi wa Liverpool wa mabao 4-3 nyumbani, Klopp alimshutumu mwamuzi, Tierney kwa kuwa na kitu "dhidi" ya Liverpool.

FA ilisema mechi ya kwanza ya marufuku ya Klopp ya kufungiwa kwa laini ya kugusa ilianza mara moja na ya pili ilisimamishwa hadi mwisho wa msimu wa 2023-24, kwa sharti hatakiuka tena Sheria ya FA ya E3 kwa sasa.

Uamuzi huo unamaanisha Mjerumani huyo hatoisimamia timu yake leo watakapoikaribisha Aston Villa.

Liverpool iko katika nafasi ya tano kwenye msimamo wa ligi wakiwa na pointi 65, pointi saba mbele ya Brighton & Hove Albion walio nafasi ya sita lakini wamecheza mechi mbili zaidi.



# 65,687/-

# MWANJA, MARANGWI WASHINDI JACKPOT BONUS MID- WEEK

**Na Mwandishi Wetu**

MKAZI wa Kata ya Kituntu, mkoani Singida, Jumanne IddI Mwanja, amejishindia Sh. milioni 5.3 katika Jackpot Bonus ya Mid-Week wakati Hussein Marangwi, ambaye ameibuka mshindi wa Supa Jackpot bonus kutoka Gongo la Mboto, Dar es Salaam amepata kitita cha Sh. milioni 4.6.

Wakizungumza katika ofisi za SportPesa baada ya uhakiki na makabidhiano wa mfano wa hundi wachezaji hao walisema wamefurahi kushinda Jackpot bonas na ni mara yao ya kwanza kushinda viwango vya zawadi ya Jackpot.

"Mimi nilianza kucheza SportPesa mwaka jana. Nakumbuka ilikuwa mwezi wa tatu baada ya kuona washindi mbalimbali wakitangazwa. Pia kulitokea msukumo mwingine pale ninapoishi kulitokea washindi ambao nilikuwa nawafahamu".

Anaendnelea kwa kusema baada ya kuhamasika ilibidi aombe msaada wa kueleweshwa namna ya kujisajili, kuweka pesa na kucheza.

Hussein alianza kucheza na SportPesa mwaka jana anaeleza aliifahamu SportPesa siku nyingi kupitia jezi za Simba kwa kuwa yeye ni mpenzi wa timu hiyo kindaki ndaki na huwa ananunua jezi kila msimu.

"Nilipowafuatilia nilibaini ni kampuni ya ubashiri na imekuwa ikitangaza washindi mara kwa mara ambao niliwaona kwenye mitandao ya kijamii."

Aliongeza wakati anaanza alikuwa anacheza Sh. 300 mechi kuanzia 12 mpaka 15. Katika kipindi hicho baada ya kujifunza namna ya kucheza.

"Namshukuru Mungu wakati naanza mwaka jana nilipata bahati ya kushinda hela nyingi kidogo kulinganisha na kiwango nilichokuwa naweka kama dau la kila mkeka niliokuwa nacheza. Najua huwezi amini lakini mara ya kwanza mimi kushinda ilikuwa katika mkeka wa multibet.

Niliweka dau la Sh. 300 na kucheza mkeka wa mechi 12 na kushinda Sh .700,000. Nilishinda tena Shs.500,000 kwa 1000 katika mkeka wa mechi za kawaida. Hapa unaweza kuona mtiririko wa ushindi wangu ulivyo kuwa.

Bahati yangu haikuishia hapo nilikuja kushinda tena Sh. 200,000 baada ya kuweka Sh. 500 kwenye mkeka wa mechi saba."

Kuhusu mikeka yao ya Jackpot waliyoshinda anasema yeye kwanza huwa na kawaida ya kuchambua mikeka kwa siku mbili kabla hajaiweka rasmi.

Wakimalizia washindi wote wawili wanawashauri Watanzania kuiamini na kucheza na SportPesa ili waweze na wao kushinda zawadi kama ambavyo wao wameweza kushinda bonus za Mid-Week na Supa Jackpot.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa SportPesa, Sabrina Msuya, aliwapongeza washindi wote kwa ushindi wao na kuwataka waendelee kucheza ili waweze kuja kushinda Jackpot yenyewe katika siku za mbeleni.

"Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza kwa kushinda Mid-Week Jackpot bonus na Supa Jackpot bonus na pia nawapenda kuwaasa endeleeni kucheza kwani ushindi hauna mwenyewe, ni juhudu yako kucheza kila mara utakapopata nafasi na hauwezi jua mnaweza kurudi tena kukabidhiwa Jackpot kamili.

Kwa watanzania nawaomba waendelee kucheza na Sportpesa kwani kila wiki washindi wa viwango mbali mbali wanapatikana". alisema Sabrina.

Wiki hii Supa Jackpot imesimamia Sh. 1,114,965,687.




# *Mayele: Inawezekana kubeba ubingwa CAF*

INATOKA UK 24

funga goli katika mechi ya marudiano, alifarijika na anataka kuacha historia ndani ya Yanga pamoja na kutangaza jina lake duniani kupitia mpira.

"Katika Ligi Kuu Tanzania Bara nimefanya kazi kubwa sana kwa kushirikiana na wachezaji wenzangu, malengo yangu ni kuiendeleza kasi hiyo kimataifa, ninaamini tunaweza," alisema.

Mkongomani huyo aliongeza anafahamu mchezo wao wa kwanza wa fainali utakuwa mgumu na wenye ushindani lakini kwa pamoja wachezaji wamejipanga kupambana ili kuhakikisha wanapata ushindi kwenye uwanja wa nyumbani.

"Nitaipambania timu yangu nikiwa na malengo ya kuisaidia kupata ushindi tukiwa hapa nyumbani pamoja na kwenye mchezo wa marudiano ambao tutaucheza ugenini, tunawaomba Watanzania waendelee kutuombea ili tufanye vizuri katika hatua hii ya fainali," Mkongomani huyo alisema.

Aliweka wazi pia amefurahi kusikia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ameongeza dau la zawadi hali inayowaongezea morali ya kupambana.

"Siri ya mafanikio yangu inatokana na nidhamu niliyokuwa nayo ikiwamo kufuata vyema maelekezo ninayopewa na benchi lake la ufundi. Ninawashukuru Watanzania kwa ushirikiano wanaoendelea kutuonyesha katika michezo yetu yote," aliongeza mshambuliaji huyo.

# Golikipa Vipers kumrithi Manula

INATOKA UK 24

Amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kutohofia na wajipange kuona timu yenye ubora mkubwa katika msimu ujao baada ya kumaliza msimu wa pili mfululizo bila ya kutwaa kombe lolote, lakini pia ikiishia hatua ya robo fainali katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.


## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 20/05/23 | 17:00 | Fulham FC vs Crystal Palace | 2.33 | 3.30 | 2.80 |
| 02. 20/05/23 | 17:00 | Wolverhampton Wanderers vs Everton FC | 2.55 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 20/05/23 | 17:30 | FC Arouca vs GD Chaves | 2.44 | 3.25 | 2.70 |
| 04. 20/05/23 | 18:00 | FC Nantes vs Montpellier HSC | 2.12 | 3.40 | 3.10 |
| 05. 20/05/23 | 19:15 | KVC Westerlo vs Standard Liege | 2.27 | 3.20 | 2.60 |
| 06. 20/05/23 | 22:00 | Lille OSC vs Olympique Marseille | 2.25 | 3.45 | 2.80 |
| 07. 21/05/23 | 00:30 | Botafogo FR RJ vs Fluminense FC RJ | 2.65 | 3.30 | 2.44 |
| 08. 21/05/23 | 00:30 | America FC MG vs Fortaleza EC CE | 2.45 | 3.40 | 2.60 |
| 09. 21/05/23 | 14:30 | Club Brugge vs Royal Antwerp FC | 2.23 | 3.20 | 2.65 |
| 10. 21/05/23 | 15:30 | SK Rapid Wien vs LASK | 2.33 | 3.20 | 2.50 |
| 11. 21/05/23 | 15:30 | West Ham United vs Leeds United | 2.22 | 3.35 | 2.95 |
| 12. 21/05/23 | 16:30 | FSV Mainz vs VfB Stuttgart | 2.35 | 3.40 | 2.70 |
| 13. 21/05/23 | 19:00 | SSC Napoli vs Inter Milano | 2.90 | 3.25 | 2.28 |
| 14. 21/05/23 | 19:00 | Adana Demirspor vs Besiktas Istanbul | 2.48 | 3.30 | 2.29 |
| 15. 21/05/23 | 19:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.17 | 3.20 | 2.75 |
| 16. 21/05/23 | 21:30 | CA Belgrano vs CA Talleres de Cordoba | 2.95 | 2.85 | 2.22 |
| 17. 21/05/23 | 22:30 | Sporting Lisbon vs Benfica Lisbon | 2.48 | 3.45 | 2.50 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAMOSI - 20/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2303 | Tottenham vs Brentford | 1.79 | 3.70 | 3.85 |
| 15:00 | 5520 | Girona vs Villarreal | 2.80 | 3.50 | 2.24 |
| 16:00 | 1041 | Kaizer Chiefs vs Cape Town City | 2.09 | 3.20 | 3.36 |
| 16:00 | 1629 | Moroka Swallows FC vs Marumo Gallants FC | 3.30 | 2.83 | 2.31 |
| 16:00 | 2055 | Sekhukhune United vs SuperSport Utd | 3.80 | 2.92 | 2.06 |
| 16:00 | 2547 | Stellenbosch vs TS Galaxy FC | 2.09 | 2.99 | 3.62 |
| 16:00 | 4442 | Kasimpasa vs Istanbulspor | 1.89 | 3.57 | 3.62 |
| 16:00 | 4684 | Cremonese vs Bologna | 2.85 | 3.20 | 2.35 |
| 16:00 | 4823 | Amazulu vs Orlando Pirates | 4.03 | 3.30 | 1.85 |
| 16:00 | 4955 | Richards Bay FC vs Bloemfontein Celtic | 2.23 | 2.92 | 3.34 |
| 16:00 | 5045 | Mamelodi Sundowns vs Wydad Casablanca | 2.06 | 2.74 | 3.87 |
| 16:30 | 1597 | Schalke 04 vs Eintracht Frankfurt | 2.75 | 3.56 | 2.24 |
| 16:30 | 1647 | Gazovik Orenburg vs Zenit St Petersburg | 3.41 | 3.93 | 1.84 |
| 16:30 | 1841 | Hoffenheim vs Union Berlin | 2.44 | 3.24 | 2.69 |
| 16:30 | 4510 | Hertha BSC vs VfL Bochum | 2.18 | 3.56 | 2.86 |
| 16:30 | 5047 | Werder Bremen vs FC Koln | 2.51 | 3.41 | 2.51 |
| 16:30 | 5202 | Torpedo Moscow vs Dinamo Moscow | 5.22 | 4.12 | 1.52 |
| 16:30 | 5863 | Santa Clara vs Portimonense | 1.94 | 3.46 | 3.57 |
| 17:00 | 1001 | Carlisle vs Bradford City | 2.07 | 3.17 | 3.32 |
| 17:00 | 1712 | Kilmarnock vs St Johnstone | 2.05 | 3.25 | 3.46 |
| 17:00 | 1809 | Wolverhampton vs Everton | 2.61 | 3.26 | 2.51 |
| 17:00 | 1886 | Fulham vs Crystal Palace | 2.35 | 3.31 | 2.76 |
| 17:00 | 3578 | Liverpool vs Aston Villa | 1.50 | 4.26 | 5.31 |
| 17:00 | 3590 | Motherwell vs Ross County | 2.15 | 3.31 | 3.15 |
| 17:00 | 5023 | Celtic vs St Mirren | 1.17 | 6.51 | 13.65 |
| 17:00 | 5537 | Bournemouth vs Manchester Utd | 5.12 | 4.17 | 1.53 |
| 17:15 | 3978 | Athletic Bilbao vs Celta Vigo | 1.65 | 3.64 | 4.79 |
| 17:30 | 5840 | FC Arouca vs GD Chaves | 2.19 | 3.31 | 3.06 |
| 18:00 | 4076 | Nantes vs Montpellier | 2.12 | 3.40 | 3.10 |
| 19:00 | 1953 | Kayserispor vs Alanyaspor | 2.08 | 3.53 | 3.11 |
| 19:00 | 3320 | Atalanta vs Verona | 1.52 | 3.95 | 5.60 |
| 19:00 | 3395 | Slavia Prague vs Viktoria Plzen | 1.50 | 4.22 | 5.70 |
| 19:00 | 4469 | Galatasaray vs Sivasspor | 1.32 | 5.15 | 7.36 |
| 19:00 | 4855 | Aris Limassol vs Omonia Nicosia | 1.40 | 4.44 | 7.19 |
| 19:00 | 4985 | Akhmat Grozny vs FK Khimki | 1.55 | 4.08 | 5.02 |
| 19:00 | 5306 | FC Wil vs FC Vaduz | 1.63 | 3.70 | 4.41 |
| 19:15 | 3663 | KVC Westerlo vs Standard Liege | 2.36 | 3.41 | 2.72 |
| 19:30 | 2393 | Almeria vs Mallorca | 2.27 | 3.15 | 3.00 |
| 19:30 | 3330 | Bayern Munchen vs RB Leipzig | 1.54 | 4.37 | 4.75 |
| 19:30 | 3339 | Getafe vs Elche | 1.47 | 3.89 | 6.59 |
| 19:30 | 4871 | Nottingham vs Arsenal | 4.73 | 3.98 | 1.59 |
| 20:00 | 4677 | Boavista vs Sporting Braga | 5.03 | 4.23 | 1.54 |
| 20:30 | 2502 | Hapoel Beer Sheva vs Maccabi Netanya | 1.53 | 3.91 | 4.94 |
| 20:30 | 3422 | Sepsi Osk vs CFR Cluj | 4.69 | 3.65 | 1.66 |
| 21:30 | 4444 | FC Luzern vs St. Gallen | 1.95 | 3.72 | 3.30 |
| 21:45 | 2813 | AC Milan vs Sampdoria | 1.17 | 6.19 | 13.97 |
| 21:45 | 3048 | KAA Gent vs Cercle Brugge | 1.71 | 3.73 | 4.30 |
| 22:00 | 1933 | Lille vs Marseille | 2.36 | 3.46 | 2.66 |
| 22:00 | 4556 | Barcelona vs Real Sociedad | 1.87 | 3.41 | 3.84 |
| 22:30 | 1807 | Famalicao vs Porto | 6.02 | 4.41 | 1.44 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Mei 20, 2023




Mourinho: Sifa wanastahili wachezaji UK. 21



Straika wa Yanga, Fiston Mayele (kulia), akiwa na Salum Abubakary wakati wakirejea nchini kutoka Afrika Kusini walipowafuata Marumo Gallants katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika. Yanga imetinga fainali ya michuano hiyo. **PICHA: MTANDAO**

# MAYELE: INAWEZEKANA KUBEBA UBINGWA CAF

**Adam Fungamwangwo na Shufaa Lyimo**

## Asema Yanga ina uwezo na ni ndoto yao kuweka historia ya...

WAKATI kikosi cha Yanga kikirejea salama nchini kikitokea Afrika Kusini, mshambuliaji nyota wa timu hiyo, Fiston Mayele, amesema ndoto yake sasa ni kuona wanatwaa ubingwa wa Kombe la Shirikisho Afrika msimu huu.

**Yanga imetinga fainali za mashindano hayo baada ya kuiondoa Marumo Gallants ya Afrika Kusini wakati USM Alger ya Algeria wao wameitoa ASEC Mimosas kutoka Ivory Coast.**

Akizungumza na Nipashe jana, Mayele, alisema inawezekana Yanga kutwaa ubingwa wa michuano hiyo ya kimataifa kutokana na wachezaji wa timu hiyo kuwa na viwango vikubwa.

Mayele alisema amejiandaa kuendeleza ushindani katika mchezo wa fainali ya dhidi ya USM Alger utakaochezwa Mei 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

"Nilishasema tangu Lubumbashi (DRC), katika mechi dhidi ya TP Mazembe hatuwezi kuishia robo fainali, leo (sasa), tuko fainali, tumefanikiwa kwa sababu kikosi chetu kina wachezaji wakubwa, nyinyi wenyewe mmeona, tunavyocheza kwenye Ligi Kuu na michuano hii ni tofauti, tuko kwenye fainali ni furaha na shangwe. Kwenye ligi ya ndani nimeshaonyesha vitu vingi.

Sasa nilitaka kuonyesha katika michuano ya kimataifa, mchezaji mkubwa unatakiwa kufanya vyema katika mechi kubwa pia. Mimi nataka kupambania timu yangu ili tuchukue kombe, ingawa USM Alger ni timu nzuri kwa sababu pia imefika fainali, kikubwa ni kufanya vyema katika mechi ya kwanza," alisema Mayele.

Aliongeza amefurahi timu yake kukata tiketi ya kucheza fainali katika mashindano hayo msimu huu na anaamini wataendelea kufanya vyema kwenye mchezo wao unaofuata.

Mshambuliaji huyo alisema amepanga kuonyesha kiwango kikubwa ili kuisaidia Yanga kutwaa ubingwa wa michuano hiyo kwa mara ya kwanza.

"Tunashukuru tumefanikiwa kuingia kwenye hatua ya fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuiondoa Marumo Gallants katika hatua ya nusu fainali, sasa tunahitaji kuendeleza ushindi kwenye mechi inayofuata," Mayele alisema.

Nyota huyo alisema mara baada ya ku-

INAENDELEA UK 23

# Golikipa Vipers kumrithi Manula

**Na Adam Fungamwango**

BIASHARA asubuhi, ndio maneno ya mabosi wa Simba ambao timu yao imeshindwa kufikia malengo msimu huu kwa kuanza mchakato wa usajili wa wachezaji wapya mapema lakini pia wakiweka wazi straika, Moses Phiri, haondoki.

Taarifa kutoka Simba zinasema tayari mazungumzo na baadhi ya wachezaji akiwamo winga, Martin Kiiza, golikipa Alfred Mudekereza wote wa Vipers ya Uganda na Sospeter Bajana wa Azam FC yameshaanza.

Mudekereza anapewa nafasi ya kumrithi kipa, Aishi Manula, ambaye huenda akapoteza namba yake katika kikosi cha Simba msimu ujao.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, aliliambia Nipashe jana wameshaanza mchakato wa usajili kwa lengo la kuboresha kikosi chake ili kiwe cha 'kutisha' katika msimu ujao na kurejesha ubabe wake.

Ahmed alisema wanasubiri ripoti rasmi ya Kocha Mkuu, Roberto Oliveira 'Robertinho' baada ya kumalizika kwa Ligi Kuu Bara lakini akiweka wazi Mzambia Phiri ataendelea kubakia klabuni hapo na si kweli ameandika barua ya kutaka kuondoka.

"Tunakisuka kikosi chetu, tunafanya maboresho pale ambapo panahitajika kufanya kwa ajili ya msimu ujao, ninavyokwambia wataalamu wetu wametawanyika sehemu mbalimbali Afrika na dunia kuangalia nani aingie kwa ajili ya kukiimarisha kikosi.

Maeneo gani yanatakiwa kuongezewa nguvu na nini tufanye kwa ajili ya kushinda makombe, baada hapo sasa tunashusha wale ambao tayari tumeshakubaliana nao," alisema Ahmed.

Aliongeza Phiri alishindwa kuhimili mikiki mikiki kutokana na majeraha aliyopata na hivyo mwalimu akawa anampa muda kidogo wa kucheza kwa ajili ya kutafuta utimamu wa mwili, sasa anaendelea kuimarika na msimu ujao anatarajiwa kurejea akiwa fiti zaidi.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >